# Nipashe

Ijumaa Machi 29, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579878

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Membe aibuka kortini kesi ya fidia bilioni 10/-

UKURASA 3



Umemejua Korogwe ulivyowapaisha kinamama kuelekea maisha mbadala Ukurasa 14

BIASHARA

BUFE

Ijumaa MACHI 29, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Kagame ang'aka namna Afrika inavyojimaliza kupitia biashara Ukurasa 19

Ulemavu ghafla ulimgeuza mjamzito tegemezi, sasa anahudumia kundi Ukurasa 16

UCHUMI ZAIDI Ukurasa 18

Takwimu za Uchumi Ukurasa 20

UKURASA 13

# JPM asimulia alivyofanikisha kunaswa watuhumiwa rushwa

**Asema** alitaka wakamatwe wakiwa ndani ya magwanda ya CCM, aanika alivyookoa mamilioni uchoraji twiga... **uk. 2**




Rais John Magufuli akishuka katika ndege aina ya Foker 50 iliyokuwa ikitumika kubeba viongozi wa serikali, ambayo kwa sasa itatumika kubeba abiria wa kawaida katika mikoa mbalimbali. **PICHA: IKULU**

## Simulizi Mkenya kutekwa kimafia

UKURASA 11

## Sheria ya habari yapigwa kumbo

**Mahakama** EAC yataka vipengele kandamizi uhuru wa habari kufutwa... **uk. 2**

**MICHEZO** AJIBU KUIKOSA ALLIANCE KESHO UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# ... Afichua alivyookoa mamilioni uchoraji twiga

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameeleza alivyookoa mamilioni ya shilingi baada ya 'wajanja' kutaka kutumia zaidi ya Sh. milioni 200 kuipeleka ndege nje ya nchi kupakwa rangi na kuchorwa picha ya twiga.

Rais Magufuli, maarufu JPM, alifichua mpango huo wa upigaji alipozungumza Ikulu jijini Dar es Salaam jana, wakati akipokea ripoti kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na kumwapisha balozi mpya wa Tanzania nchini Cuba, Valentino Mlowola.

Alisema kulikuwa na mpango wa kuisafirisha ndege iliyokuwa inatumiwa na Rais kwenda nje ya nchi kupakwa rangi na kuchorwa nembo ya mnyama twiga ili ianze kutumiwa na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kubeba abiria.

"Kuna siku nilikuwa kwenye sherehe uwanja wa ndege, nikaagiza ndege ya Rais ipelekwe ATCL ili ikasaidie kubeba watu, agizo hilo likapokelewa, likabaki suala la kubadilisha maneno, kuyatoa yale maneno

INAENDELEA UK. 3



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipokea zawadi kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya TPB, Dk. Edmund Mndolwa, baada ya kuzindua akaunti mpya ya benki hiyo, maalum kwa kinamama iitwayo Tabasamu, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPB, Sabasaba Moshingi na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji. **PICHA: JOHN BADI**

# JPM asimulia alivyofanikisha kunaswa watuhumiwa rushwa

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesimulia namna alivyofanikisha kukamatwa kwa 'vigogo' wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliokuwa wakiomba rushwa ya shilingi milioni tano kwa mfanyabiashara ili waweze kumpangisha kwenye jengo la CCM.

Mwanzoni mwa wiki hii, Takukuru iliwafikisha mahakamani viongozi watatu wa CCM wakituhumiwa kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

Washtakiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, wakishtakiwa kwa vitendo vya kuomba na kupokea rushwa kwa ajili ya kutoa eneo la kupanga katika jengo linalomilikiwa na CCM.

Washtakiwa hao ni Jenifer Lemunge, ambaye ni Katibu wa CCM Tawi la Amana, Katibu Kata wa CCM Ilala, Devotha Bantulaki na Frank Joseph ambaye ni Katibu wa Hamasa wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza jana, Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya kumwapisha balozi mpya wa Tanzania nchini Cuba, Valentino Mlowola, pamoja na kupokea ripoti ya utendaji wa Takukuru, Rais Magufuli alisema yeye ndiye aliyewapa taarifa Takukuru kuwapo kwa watu hao, baada ya kupigiwa simu na raia aliyekuwa anaombwa rushwa.

"Hivi karibuni nilipigiwa simu na raia kwamba anaombwa rushwa ya shilingi milioni tano na viongozi wa CCM ili wampangishe majengo yao yaliyopo Ilala na walisema alipe fedha hizo kwa sababu ndiyo kula yao," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Nikasema kwa nini hamkwenda Takukuru, wakasema hawapatikani na anaogopa wanaweza kumjua. Nikajaribu kumtafuta kiongozi wa CCM wa Dar es Salaam sikujua namba yake, nikamtafuta Mkurugenzi mmoja Takukuru nikamwambia shughulikia suala hili na nikamwambia ahakikishe watu hao wanakamatwa," alisema Rais Magufuli na kuongeza.

"Nikamwambia awashike tena wakiwa wamevaa nguo za kijani na kweli baada ya saa mbili wakawa wameshikwa. Akashikwa mmoja akawapigia wenzake kuwa wameshapata mgawo, wakasema

INAENDELEA UK. 8


# Tanpack Tissues Limited

## PAPER TO DISPOSE?

Recycle Paper, Reduce Pollution, Conserve Environment



Offering Secured Document Destruction & Recycling Solutions for Various Grades of Paper

Partner with us for Recycling
Contact us :

DAR ES SALAAM
Mr. Deep Parmar
82 Soldering road, Mikocheni B, Opp. Sayona
Tel (Gen): +255 22 2773001/3
(Mob): +255 712 424738

ARUSHA
Mr. Suresh Kalyani
Factory Area, Unga Road
Tel (Mob): +255 754 817400

115104002


# Sheria ya habari yapigwa kumbo


## ANATAFUTWA NA MWAJIRI WAKE



Jina: SAID KANYANI

Mtajwa hapo juu (Pichani) ni Mwajiriwa wa Kampuni ya **IMANI SUPERDEALER CO LTD** iliyopo Kinondoni B, Dar es salaam. Amemuibia mwajiri wake na kukimbilia kusikojulikana.

Atakayemuona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. **URP/RB/300/2018 – *WIZI au apige simu namba 0754 421651.***

***Donge nono litatolewa kwa atakayefanikisha kukamatwa kwake.***

MKURUGENZI WA KAMPUNI.

215144902


**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WADAU wa habari wamesema demokrasia, uhuru wa habari, uhuru wa kujieleza umeshinda kwa Watanzania, baada ya jana Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ) kusema Sheria ya Huduma ya Habari 2016 inakiuka misingi ya Sheria ya Mkataba unaounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo kuitaka serikali kuifanyia marekebisho.

Katika hukumu iliyotolewa jijini hapa jana, Jaji Charles Nyachae, aliamuru vifungu 7(3)(a), (b), (c),(f),(g),(h),(i), na (j); vifungo 19, 20 na 21; vifungu 35; na vifungu 58 na 59 vya sheria hiyo vinakiuka Ibara 6(d) ya Sheria ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aidha, aliagiza Serikali ya Tanzania inaelekezwa kuchukua hatua za lazima kuhusu Sheria ya Huduma ya Habari ili iendane na misingi ya mkataba wa EAC.

Mahakama hiyo imesema kila upande utatakiwa kulipa gharama za kesi hiyo wenyewe.

Akiwa na majaji Monica Mugenyi na Audace Ngiye, Jaji Nyachae, alisema, mahakama imeridhika

INAENDELEA UK. 8

## ... Afichua

INATOKA UK. 2

Air Tanzania na kuchora nembo ya twiga," alisema.

Rais Magufuli aliongeza: "Wakasema haya maneno kuyaandika na kuchora twiga hayawezi kufanyika Tanzania, hayupo mtu wa kufanya hivi, zikatafutwa nchi tatu za nje zinazoweza kufanya hiyo kazi, sitaki kuzitaja.

"Nikasema jamani hapana, tafuteni wataalamu wenu hapahapa nchini wanaojua kuchora, watashindwa kuchora twiga kweli!

"Mbona wanajua kuchora simba? Wakakaa kimya wakifikiri nimesahau, wakawa wametafuta nchi fulani kimyakimya ili waipeleke hiyo ndege.

"Baadaye Jumapili moja nikaambiwa 'ile ndege inaondoka kesho', nikaambiwa watakaoisindikiza hiyo ndege wameshalipwa dola 28,000 (Sh. milioni 65.346) na malipo ya awali ya asilimia 60 yameshalipwa kule zinakopelekwa, gharama kama Sh. milioni 200 hivi. Na wasindikizaji wameshaandaliwa, wapo hadi wahudumu wa ndege.

"Nikajiuliza ndege inakwenda gereji, sasa hawa wahudumu wanakwenda kumhudumia nani? Na siku za ukarabati zilizopangwa zilikuwa 15 hadi 30, nazo zikiwa zimelipiwa ili wakati ndege inapakwa, wawe wanaisubiri.

"Nikasema hii ndege ikiondoka, hao wote waliohusika wanaondoka saa hiyohiyo, ikiwa inapaa na wao wanaondoka."

Alisema baada ya kutoa tahadhari hiyo, ndege haikuondoka na ikapakwa rangi nchini kwa gharama ya Sh. milioni tano, huku ikiwa na nembo ya twiga na maneno ya Air Tanzania.

Jana mchana, Rais Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza kukagua kazi ya kupaka rangi ndege ya Foker 50 iliyokuwa ikitumiwa kubeba viongozi ambayo itaanza kubeba abiria.

Rais Magufuli alikutana na kufanya mazungumzo na mafundi wazalendo ambao walifanya kazi hiyo ya kuchora mnyama twiga na kupaka rangi ndege hiyo kwa gharama ya Sh. milioni saba.

Baada ya kufanya ukaguzi huo, Rais Magufuli aliwazawadia mafundi waliofanya kazi hiyo Sh. milioni 10 kutokana na kazi nzuri waliyoifanya.

Akiwa Ikulu, Rais Magufuli pia alizungumzia changamoto ya rushwa nchini, akieleza kuwa ni jambo ambalo haliwezi kukubalika mahali popote kwa kuwa linaondoa amani, haki, maendeleo na kukimbiza wawekezaji.

"Tunafahamu kuna wawekezaji walishindwa kuwekeza hapa nchini kwa sababu waliombwa rushwa, wakaenda kuwekeza nchi zingine," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli pia alisema nchi inaibiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na udanganyifu kwenye kodi, akitolea mfano marejesho

INAENDELEA UK. 8

# Waziri wa JK atinga kortini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, jana alitinga Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, kusikiliza kesi yake ya madai fidia ya Sh. bilioni 10 dhidi ya Cyprian Musiba iliyopangwa kusikilizwa mahakamani hapo.

Hata hivyo, mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Elinaza Luvanda, ilishindwa kuanza kusikiliza madai hayo baada ya mlalamikiwa kuwasilisha maombi ya kuomba kuongezewa muda wa kuwasilisha majibu dhidi ya Membe.

Membe aliyekuwa ametinga mahakamani hapo akiwa amevaa shati jeupe na suruali nyeusi, alifika mapema saa 3:00 asubuhi akiwa na wakili wake, Jonathan Mndeme.

Upande wa mlalamikiwa uliwasilisha maombi namba 119/2019 ya kuomba kuongezewa muda wa kuwasilisha majibu nje ya muda.

Jaji alisema mlalamikaji atawasilisha majibu ya maombi hayo Aprili 12 na mahakama yake itasikiliza Aprili 17, mwaka huu na kwamba kesi ya msingi itasubiri uamuzi wa maombi hayo utakapotolewa.

Musiba anadaiwa kumtuhumu Membe kuwa anamhujumu Rais John Magufuli, na kwamba mbinu mojawapo ya kukamilisha hujuma hizo ni maandalizi ya kampeni za kugombea urais 2020.

Membe alikuwa mmoja wa wanachama 38 wa CCM waliowania kuteuliwa kugombea urais kupitia chama hicho katika uchaguzi mkuu wa 2015.

Hata hivyo, katika kinyang'anyiro hicho, alifikia hatua ya tano bora katika ngazi ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) sambamba na Magufuli, January Makamba, Dk. Asha Rose Migiro na Balozi Amina Salum Ali.

Kabla ya kinyang'anyiro hicho, Membe alikuwa Mbunge wa Mtama kwa miaka 15 na katika serikali ya Kikwete (mwaka 2006 hadi 2015) alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Nishati na Madini na hatimaye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa miaka minane.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## UNAUDITED RESULTS
### FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

The year of 2018 saw continued growth in the local cement industry, with the market increasing at a higher rate than in previous years. Competition was again fierce, and yet despite the cement over capacity in the local market, TPCPLC once again strengthened its market leadership.

The efforts made throughout the year on the operational side to increase clinker production, whilst overcoming technical challenges, combined with the focus on producing and selling high quality products, whilst maintaining strong customer relationships and service excellence, has allowed TPCPLC to report an improved full year result.

Total volumes sold in 2018 increased by 9% on 2017, and with revenue also increasing by 30%, this resulted in an operating profit of TZS 80.1Bn being recorded, a 28% increase on the previous full year result.

| INCOME STATEMENT | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 348,863,384 | 268,209,096 |
| Cost of sales | (223,951,693) | (184,903,676) |
| **Gross profit** | **124,911,691** | **83,305,420** |
| Selling and administrative expenses | (27,221,412) | (25,029,949) |
| Other operating income | 148,927 | 22,463,707 |
| Depreciation and amortization | (17,778,169) | (18,066,388) |
| **Operating profit** | **80,061,037** | **62,672,790** |
| Financial items | 1,683,745 | 2,925,035 |
| **Profit before tax** | **81,744,782** | **65,597,825** |
| Taxes on income | (24,878,688) | (30,001,432) |
| **Net profit for the period** | **56,866,094** | **35,596,393** |
| Other comprehensive income, net of tax | (403,822) | (1,362,319) |
| **Total comprehensive income** | **56,462,272** | **34,234,074** |
| Number of shares | 179,923,100 | 179,923,100 |

| BALANCE SHEET | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| **Assets** | | |
| Intangible fixed assets | 1,304,535 | 2,635,382 |
| Tangible fixed assets | 140,948,038 | 150,539,114 |
| Non-current financial assets | 7,513,661 | 16,743,912 |
| **Non current assets** | **149,766,234** | **169,918,408** |
| Inventories | 55,104,226 | 41,711,115 |
| Trade and other receivables | 44,712,022 | 37,662,987 |
| Other current financial assets | 7,191,031 | 4,119,985 |
| Cash and cash equivalents | 65,987,258 | 34,739,002 |
| **Currents assets** | **172,994,537** | **118,233,089** |
| **Total assets** | **322,760,771** | **288,151,497** |
| **Equity and Liabilities** | | |
| **Equity** | **224,935,758** | **186,465,797** |
| Long term provisions | 8,205,223 | 6,867,069 |
| Provision for deferred taxes | 21,035,003 | 25,220,943 |
| **Non current liabilities** | **29,240,226** | **32,088,012** |
| Dividend payable | 3,850,962 | 15,519,795 |
| Trade and other payables | 61,158,067 | 45,643,564 |
| Taxes payables | 3,575,758 | 8,434,329 |
| **Current liabilities** | **68,584,787** | **69,597,688** |
| **Total equity and liabilities** | **322,760,771** | **288,151,497** |

**Prospects**
The company continues to face increasing competition, but TPCPLC will continue to work to maintain its market leadership position.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support during the year. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders in the future.

**BY ORDER OF THE BOARD**

**Hakan Gurdal**
**Chairman of the Board**
**29 March 2019**

| STATEMENT OF CASH FLOW | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| Profit before tax | 81,744,782 | 65,597,825 |
| Depreciation and amortisation | 17,778,169 | 18,066,388 |
| Interest received | 1,350,833 | 635,206 |
| Income tax paid | (31,997,950) | (20,645,696) |
| Elimination of non cash items | (3,858,379) | (24,284,245) |
| Change in working capital | (1,175,840) | 20,457,132 |
| **Cash flow from operating activities** | **63,841,615** | **59,826,610** |
| **Cash flow from investing activities** | **(2,932,216)** | **(80,827)** |
| Dividend paid | (29,661,144) | (48,182,450) |
| **Change in cash and cash equivalents** | **31,248,256** | **11,563,333** |
| Cash and cash equivalent 01.01 | 34,739,002 | 23,175,669 |
| Change in cash | 31,248,256 | 11,563,333 |
| **Cash and cash equivalent 31.12** | **65,987,258** | **34,739,002** |

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O. Box 1950**
**Dar es Salaam**
**Tanzania.**
**Tel +255 746 810930 Fax: +255 746 810931**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**

215145302

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2018(Kiasi kwa Shilingi milioni)

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | MWAKA WA SASA 31.12.2018 | MWAKA ILIYOPITA 31.12.2017 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,744 | 5,049 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 17,681 | 18,569 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 23,368 | 17,333 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 27,511 | 38,782 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | 11 | 27 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 98,573 | 86,008 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,412 | 1,002 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,279 | 1,463 |
| # | **Jumla ya Mali** | **173,579** | **168,233** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,272 | 4,021 |
| 18 | Amana za Wateja | 132,158 | 125,592 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 137 | 129 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 41 | 154 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Z | 20 | 5 |
| 27 | Dhima Nyingine | 896 | 1,211 |
| 28 | Madeni | - | - |
| # | **JUMLA YA DHIMA** | **134,524** | **131,112** |
| # | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **39,055** | **37,121** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 937 | 781 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 21,987 | 19,436 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,147 | 2,836 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,984 | 4,067 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **39,055** | **37,120** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 7,209 | 19,340 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,567 | 9,377 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,151 | 2,611 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22% | 22% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7% | 11% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76% | 69% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 57% | 51% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86% | 84% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3% | 2% |
| (vii | Ongezeko la Mali | 3% | 6% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2018

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2017 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 13,582 | 14,177 |
| 2 | Gharama za Riba | 4,676 | 4,845 |
| **3** | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **8,906** | **9,332** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | 1,259 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 1,018 | 1,427 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **1,932** | **1,959** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 349 | 530 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,519 | 1,423 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 64 | 6 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba:** | **5,063** | **5,647** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,869 | 1,613 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 441 | 711 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 2,753 | 3,323 |
| | 7.4 Other Provision | - | - |
| **8** | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,498** | **4,217** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 1,351 | 1,381 |
| **10** | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,147** | **2,836** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **2,147** | **2,836** |
| **13** | Idadi ya Waajiriwa | **48** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 215 | 284 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7% | 10% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 47% | 22% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5% | 17% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2018

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2017 |
|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 3,498 | 4,217 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - |
| | -Hasara katika Mali | 1,246 | 1,680 |
| | -Prior Period Adjustment | (211) | - |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (13,583) | (32,568) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | (4) | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 6,566 | 2,561 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (3,157) | 2,639 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 7,451 | (746) |
| | -Kodi Iliyolipwa | (1,351) | (1,612) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | (400) | 1,707 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **55** | **(22,121)** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (45) | (276) |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 5 | - |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | (6,035) | 2,080 |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(6,075)** | **1,804** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** |
| **IV** | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **(6,021)** | **(20,317)** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 37,327 | 57,644 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **31,307** | **37,327** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2018

(Kiasi Kwa Shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **22,272** | **4,068** | **781** | **-** | **37,120** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,147 | - | - | - | 2,147 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (211) | - | - | - | (211) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,135** | **3,984** | **937** | **-** | **39,056** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **21,461** | **2,317** | **507** | **-** | **34,285** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,836 | - | - | - | 2,836 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,751) | 1,751 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (274) | - | 274 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **22,272** | **4,068** | **781** | **-** | **37,120** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2018**
**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir<br>(Mkurugenzi Mtendaji) | | 22nd March, 2019 |
| Deogratias Edward Ndushi<br>Mkuu wa Fedha | | 22nd March, 2019 |
| Mwita Mohamed Mwita<br>(Mkaguzi wa Ndani) | | 22nd March, 2019 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni<br>(Mkurugenzi) | | 22nd March, 2019 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava<br>(Mkurugenzi) | | 22nd March, 2019 |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# WFP imetuonyesha ushirikiano wa kweli

**TAARIFA** kwamba Tanzania imeahidiwa msaada wa chakula kutoka Umoja wa Mataifa ikiwa kutakuwapo na uhaba, ni jambo jema na kudhihirisha ushirikiano na uhusiano wa dhati.

Katika toleo letu la jana, tuliripoti kwamba Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP), limesema kwamba lipo tayari kuisaidia Tanzania muda wowote endapo itakumbwa na ukame au uhaba wa chakula, kama ilivyo sasa kwa Kenya.

Mwakilishi Mkazi wa WFP Tanzania, Michael Dunford, ndiye aliyetoa ahadi hiyo juzi, jijini Dar es Salaam, alipokutana na waandishi wa habari kuzungumzia upatikanaji wa lishe bora katika wilaya za Chamwino, Bahi, Ikungi zilizoko kwenye mikoa ya Dodoma na Singida, baada ya kuzitembelea na kufanya utafiti.

Dunford alisema kwamba WFP wana utaratibu wa kusaidia linapotokea tatizo la ukame au janga la njaa katika nchi husika, kama ilivyo sasa katika nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe ambazo zimekumbwa na mafuriko.

Dunford alibainisha kuwa shirika lake limeshatoa msaada kwa nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe, na kuwa kuna timu yao ambayo imekwenda katika nchi hizo kwa lengo la kusaidia.

Kwa mujibu wa mwakilishi huyo, WFP itasaidia maeneo yoyote yenye ukame Afrika Mashariki kama vile eneo la Turkana Kenya ambalo kwa sasa limekumbwa na ukame mkubwa.

Ahadi ya utayari wa WFP kuisaidia Tanzania ikiwa itakumbwa na changamoto ya uhaba wa chakula, tunaamini kuwa imetokana na nchi yetu kuaminiwa na shirika hilo kutokana na umakini katika ushiriki wa shughuli za Umoja wa Mataifa yakiwamo masuala ya chakula.

Katika kuonyesha uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo, hivi karibuni tuliona jinsi shirika hilo lilivyotangaza kununua tani kadhaa za chakula kutoka Wakala wa Chakula wa Taifa (NFRA), lengo likiwa ni kuhakikisha mazao ya chakula yanayozalishwa na wakulima wetu nchini hususan mahindi yanapata soko la uhakika. Kadhalika, shirika hilo limekuwa likitoa na kusafirisha chakula katika kambi za wakimbizi ambao wamekuwa wanaishi nchini kutoka katika nchi zenye migogoro.

Kadhalika, WFP kupitia programu ya boresha lishe imekuwa ikishirikiana na ngazi za juu kitaifa kama vile Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), katika kuhakikisha kwamba wananchi hususan kinamama na watoto wanapata lishe bora.

Kuna umuhimu mkubwa wa kupongeza ahadi hiyo na inadhihirisha jinsi uhusiano wa Tanzania na WFP ulivyo wa ukweli, na usioacha shaka yoyote.

Kimsingi, kauli ya Dunford inatokana na tishio kwa baadhi ya maeneo nchini kukumbwa na uhaba wa chakula kutokana na uwezekano wa kukosa mvua za masika kama ilivyo katika nchi jirani ya Kenya, ambayo imekumbwa na ukame katika maeneo kadhaa.

Kadhalika, nchi zingine jirani za Malawi, Msumbiji na Zimbabwe zimekumbwa na uhaba wa chakula kutokana na athari za kimbunga. Tunaamini kuwa uhusiano na ushirikiano mzuri na wa karibu ulioko kati ya Tanzania na WFP utaendelea na kudumishwa kwa maslahi ya pande zote.

Hilo linatokana na kauli ya Dunford kuwa, shirika hilo limekuwa likifanya kazi na Tanzania kwa muda mrefu katika kusaidia chakula, hivyo itaendelea kushirikiana katika kila jambo litakalotokea.

Tunatambua umuhimu mkubwa wa uhakika wa chakula kwa jamii yoyote kwa kuwa kinyume chake, ni vigumu kupata maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tusiendekeze mitumba hii, ni hatari kwa afya zetu

**MIAKA** zaidi ya mitano iliyopita, biashara ya nguo za ndani za mitumba ilipigwa marufuku nchini, lengo ni kulinda afya za wavaaji.

Hatua hiyo ilichukuliwa, kutekeleza matakwa ya agizo la sheria ya mwaka 2009, inayozuia matumizi ya nguo za ndani zilizokwishatumika.

Baadhi ya nguo hizo ni sidiria, mavazi ya ndani, taiti, chupi na hata soksi, inayoelezwa zimekuwa zikiuzwa kwa bei nafuu, hivyo zinachangamkiwa na wateja wengi, hasa jamii ya wenye kipato kidogo.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ndilo lililopiga marufuku nguo hizo tangu mwaka 2013 na limekuwa likitoa elimu kuhusu madhara yake kiafya, kwa wauzaji na wavaaji, lengo ni wauzaji na wateja waachane nazo.

Pamoja na juhudi hizo, bado wapo baadhi ya wafanyabiashara wanaoendelea kuingiza na kuuza nguo hizo nchini kwa 'njia za panya,' huku wateja nao wakizichangamkia, kutokana na unafuu wa bei yake.

Hali hiyo inasababisha shirika hilo kuendesha ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo masoko, maghala na kunasa marobota au nguo, ambazo huwa zimewekwa mezani tayari kwa kuuzwa.

Kwa mfano, hivi karibuni maofisa wa TBS kutoka makao makuu Dar es Salaam na watokao Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, walifanya ukaguzi wa kushtukiza katika soko la Sido jijini Mbeya na kunasa zaidi ya marobota 20 ya nguo hizo yakiuzwa.

Ofisa Uhusiano wa TBS, Rhoida Andusamile, ndiye aliyeongoza msako huo, akisema lengo ni kuhakikisha biashara ya nguo hizo za ndani zinakomeshwa nchini. Anawataka Watanzania waachae kutumia nguo za ndani mitumba.

Wafanyabiashara walionaswa na nguo hizo, wanajitetea hawajui madhara hayo kwa binadamu na awanaomba waendelee kupewa elimu, ili kuwaepusha na hasara ya kuchukuliwa mali zao. Ombi lao ni sahihi, lakini pia sidhani kwamba kwa miaka yote hiyo tangu marufuku ianze mwaka 2013 hajapewa elimu kweli? Hata kama kuna wafanyabiashara wapya, hawawezi kuelimishana wao kwa wao?

Nakumbuka wakati marufuku hiyo inatangazwa kwa mara ya kwanza, baadhi ya wafanyabiashara waliomba wapewe muda zaidi kumalizia biashara hiyo, kwa madai kwamba walikuwa na nguo nyingi.

Baada ya kuruhusiwa na kufanya hivyo, biashara ya nguo hizo haikukoma hadi leo inaendelea kuuzwa kama kawaida, kana kwamba hakuna marufuku yoyote inayohusu nguo za ndani za mitumba.

Umefika wakati sasa, wafanyabiashara na wateja wao kubadilika na kuacha 'ujanjaujanja' ambao unaishia katika hatari ya afya zao, hivyo waunge mkono juhudi zinazofanywa na TBS kukomesha biashara hiyo.

Marufuku ya nguo hizo, ni kwa ajili ya kulinda afya za Watanzania. Sasa wanapojitokeza baadhi ya wafanyabiashara wanaotumia 'njia za panya' kuziingiza nchini, maana yake ni kwamba wana nia mbaya.

Ushauri wangu ni kwa wafanyabiashara wasijali upande mmoja wa kuingiza pesa kwa wingi kupitia nguo hizo, pia wateja nao wasiangalie unafuu wa bei, bali waweke mbele usalama wa afya zao, ambao ni muhimu kuliko vinginevyo.

Kwa hiyo, ni muhimu watumiaji wafahamu madhara ya kuvaa nguo hizo za ndani zilizovaliwa na watu wengine, ambao hawawajui na wala hawajui afya zao na magonjwa, ambayo huenda wanayo.

Wataalamu wa afya wanasema, nguo za ndani za mitumba ni hatari, kwa vile zinaweza kusababisha madhara ya kudumu kwa wavaaji, kutokana na ukweli kwamba zilishavaliwa na mwingine, ambaye afya yake haijulikani.

Mkurugenzi wa Chuo cha Sayansi ya Afya Kam, Kimara Dar es Salaam, Dk. Kandore Musika, anasema mvaaji wa kwanza anaweza kuwa na magonjwa ya ngozi, fangasi, au hata ya zinaa, inayoweza kubakiza vijidudu katika nguo na kisha, vikamwingia mvaaji wa pili, hivyo kumsababishia maradhi.

Anasema, magonjwa yanayoweza kusababishwa na nguo hizo ni mengi kwa wavaaji na kwamba kugundulika kwa chanzo chake ni vigumu, hasa kwa kutokuwa na kumbukumbu ya uhalisia wa kuvaliwa kwake.

Dk. Kandore Musika, anasema njia nyingine inayoweza ikawafanya wavaaji wakawa salama, ni kuziweka nguo hizo kwenye maji yanayochemka, kuzianika juani na kisha kuzipiga pasi.

Anafafanua, kuna baadhi ya mafua yanatokana na uvaaji wa nguo za aina hizo, hasa kama zinakotoka zilivaliwa na zikawa na mchanganyiko wa harufu zinazoweza kuathiri mfumo wa upumuaji binadamu mwingine, anayezivaa baadaye.

"Ikumbukwe magonjwa mchanganyiko ya ngozi, wakati mwingine yanaweza kusababishwa na nguo mbalimbali za mitumba kama zitakuwa hazijaandaliwa kwa kuzingatia misingi ya afya kabla ya kuvaliwa," ndivyo anavyohitimisha Dk. Musika.

# UMG kuzindua 'Jukwaa la Tafakuri'

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA jipya la Tafakuri linatarajiwa kuzinduliwa kesho jijini Dar es Salaam likiwa na lengo la kujenga utaifa na kulinda uhuru wa wananchi kwa kuwarithisha vijana uhifadhi wa historia, utamaduni na rasilimali za Tanzania na Afrika.

Taarifa iliyotolewa na Uhuru Media Group (UMG) kwa vyombo vya habari jana, ilisema Watanzania pamoja na raia wa nchi mbalimbali Barani Afrika wanatarajia kunufaika na Jukwaa hilo.

Jukwaa hilo ambalo limeanzishwa na UMG kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo Hifadhi ya Taifa (Tanapa), "Dhamira yake kuu ni kuenzi na kuendeleza fikra za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alifanya kazi kubwa ya kutetea Bara la Afrika," alisema Ernest Sungura, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa UMG na kuongeza: "Moja ya mambo tutakayofanya katika Jukwaa la Tafakuri, ni kuwakutanisha vijana, hasa wa sekondari na vyuo vikuu, na wazee au watu wenye uzoefu wa kutosha kuhusu historia na urithi wa Bara la Afrika, hususan Tanzania. Hii ni fursa ya pekee kwa vijana kuibua hoja au kuuliza maswali yatakayonogesha midahalo na kutuchochea sisi kuendeleza, kutafiti na kufuatilia matukio yanayomhusu Hayati Mwalimu Nyerere na urithi wetu."

Akiongea na waandishi wa habari, Sungura alisema, shughuli ya kuzindua Jukwaa la Tafakuri la Uhuru Media Group itafanyika Machi 30, Mlimani City, katika ukumbi wa Cinemax kuanzia saa 10:30 jioni hadi saa 2:00 usiku.

Tukio hilo ambalo litaanza kwa kuangalia Makala maalum iliyoandaliwa kuhusu Mwalimu Nyerere, litazinduliwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala.

Mada ya uzinduzi wa Jukwaa hilo ni: "Muungano wetu ni Umoja wetu, Historia yetu na Urithi Wetu."

"Mada hiyo itahusishwa na Mwalimu Nyerere kwenye mdahalo huo ili vijana wetu waweze kuiga mambo mengi mazuri kutoka kwake," Sungura alisema.

Jukwaa la Tafakuri litatumia mbinu mbalimbali ili vijana wa sasa waweze kuhuhisha falsafa za kiongozi huyo mzalendo aliyekuwa na maono ambayo bado yanaishi na kuendelezwa na viongozi kama anavyofanya Rais Dk. John Magufuli, ambaye anafuata nyayo za Mwalimu kwa kuthamini utu hasa wa wanyonge, kupigania rasilimali za taifa, kusimamia haki, umoja, na kutetea uhuru wa taifa.

Aidha, Jukwaa la Tafakuri litazinduliwa pia Zanzibar kumuenzi Hayati Amani Abeid Karume, Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mwanamapinduzi asiyesahaulika kwa aliyoyatenda Zanzibar na kwa mustakabari wa Muungano wa Tanzania.

# Kesi ya kina Mbowe yashindwa kusikilizwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, jana imeshindwa kuanza kusikiliza ushahidi wa Jamhuri wa kesi ya uchochezi na kufanya mkusanyiko usio halali inayowakabili vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, baada ya Ester Bulaya kudaiwa kuwa mgonjwa.

Hata hivyo, Wakili Peter Kibatala alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba kwamba mshtakiwa Bulaya ameridhia kesi kuendelea kusikilizwa bila uwepo wake.

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
27 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATATU tarehe 01-04-2019 kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEA CONSTRUCTION & INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka SUMBAWANGA kuelekea KABANGA, gari zenye namba za usajili:

2. **T 389 BES / T 668 BCJ**
   **T 550 BES/T 474 BCJ**
   **T 349 BNT/ T 646 BCJ**

3. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita** | **20.00** |
| **Upana** | **-** | **mita** | **3.00** |
| **Kimo** | **-** | **mita** | **4.80** |

4. Njia itakayotumika :SUMBAWANGA hadi KABANGA kupitia MPANDA, Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115133502



**TUNAKUFIKIA POPOTE ULIPO TANZANIA**
**TANGAZA NASI SASA!!**






Wawakilishi wetu wa mikoani

Iringa: Siangicha Ngowi- 0658269470
Tanga: Elisha Eliya Eliya 0719923993
Arusha: Hevens Mrema – 0754481773
Zanzibar: Marry Kizuguto- 0714262437
Dodoma, Singida: Sultan Ally -0714889096 & Raymond Mushi:0784 604262
Kilimanjaro, Manyara: Kelvin Lymo- 0715840855
Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Mara, Kigoma: Abel Manase 0715214119 & Imani Isaya 0652 751 391
Morogoro: Baragash Hassan -0659324138
Ruvuma, Lindi, Mtwara : Gideoni Mwakanosya-0754928752
Rukwa, Mbeya, Njombe: Gibson Mwakatwila 0767318070
Tabora: Halima Ikunzi- 0743868485
Shinyanga: Shaaban Njia 0757209852
Pwani: Mwombeki Mbekomize 0756756122
Dar Es Salaam: Moses Masunga 0755 642851

615126102

The Guardian
Nipashe

**For More Information Please contact:**
Simu: +255 767 223 311, Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
Mikocheni Light Industrial Area
SLP 31042 Dar es Salaam



**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**TANGAZO**

**PATA KIWANJA JIJINI DODOMA**

**22/03/2019**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anapenda kuwatangazia Wananchi wote kuwa, Halmashauri imekamilisha upimaji wa viwanja vya matumizi mbalimbali katika eneo la Nala, Barabara Kuu ya Dodoma-Singida na vitauzwa kuanzia tarehe **25/03/2019** katika eneo la wazi lililopo kwenye Ofisi za Manispaa ya zamani jirani na Sabasaba.

Mchanganuo wa bei na muda wa malipo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali.

| Na. | Matumizi | Bei (kwa mita moja ya mraba) | Muda wa malipo | Eneo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Makazi | 5,000 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |
| 2 | Biashara | 6000 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |
| 3 | Makazi na Biashara | 5,500 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |
| 4 | Taasisi | 6,000 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |

Aidha, kila anayehitaji kiwanja afike katika Ofisi na tarehe tajwa hapo juu ili akamilishe taratibu za kumilikishwa kiwanja Jijini Dodoma, Makao Makuu ya Nchi. Kwa mawasiliano zaidi piga namba 0714785513.

Tangazo hili limetolewa na:

**Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji**

**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

215135802

# Sheria ya habari yapigwa kumbo

INATOKA UK. 2

Sheria ya Huduma ya Habari inakiuka misingi ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aliutaka upande wa walalamikiwa (Serikali) kuifanyia marekebisho sheria hiyo ili iweze kukidhi misingi ya mkataba unaounda EAC kwa kuwa Tanzania ni sehemu ya jumuiya hiyo.

Jaji Nyachae alisema licha ya kukiuka mikataba ya kimataifa, Sheria ya Huduma ya Habari, inakiuka misingi ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Walalamikaji katika kesi hiyo iliyofunguliwa Januari 2017 ni Baraza la Habari Tanzania, (MCT), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (HRDC) dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) aliyeshtakiwa kwa niaba ya Serikali ya Tanzania.

Katika maombi ya walalamikaji walisema kwamba chini ya mkataba wa EAC, Tanzania inapaswa kuzingatia haki za msingi kama kifungu cha 6(d) na 8(1) (c) kama zilivyoainishwa katika mkataba huo.

Walidai mlalamikiwa (Serikali) amekiuka misingi hiyo hali inayoweza kukwamisha au kuhatarisha malengo au utekelezaji wa vifungu katika mkataba huo.

Walisema sheria hiyo inaminya uhuru wa kujieleza ambao ndiyo msingi wa demokrasia, utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi na utawala bora ambao mlalamikiwa ameamua kutozingatia kwa mujibu wa Mkataba wa EAC ikiwa ni pamoja na mitakaba mingine ya kimataifa ambayo imeridhia.

### WADAU HABARI WASHANGILIA

Baada ya hukumu ya Jaji Nyachae kusomwa, wadau wa habari waliibua shangwe wakipongezana na kuwapongeza mawakili wao.

Mawakili wa walalamikaji hao walikuwa Donald Deya, Fulgence Masawe, Jenerali Ulimwengu na Jebra Kambore, wakati mawakili wa mlalamikiwa walikuwa Mark Mulwambo na Sylivia Matiku.

Akizungumza baada ya hukumu hiyo, Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema:

"Kitu cha muhimu hapa, tumeona demokrasia imeshinda, haki ya uhuru wa habari kwa Watanzania leo (jana) imethibitishwa na Mahakama ya Afrika Mashariki, haki ya waandishi wa habari kufanya kazi bila kubughudhiwa isivyo halali imethibitishwa leo (jana) na Mahakama ya Afrika Mashariki.

"Hili ni jambo kubwa sana, huu ni ushindi wa kihistoria na ni ushindi kwa kila mtu, ni ushindi kwa waandishi wa habari na ni ushindi kwa wananchi wa Tanzania mmoja mmoja na ni ushindi kwa Serikali ya Tanzania kwa sababu inapewa wasaa wa kwenda kurekebisha sheria hii ambayo vifungu vyake vingi vimeonekana vinakiuka misingi ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutoa mashariti yanayopingana na mkataba.

Kwa upande wake, Wakili Masawe, alisema, hukumu hiyo imehitimisha safari yao ndefu waliyoianza Januari, mwaka 2017 walipofungua shauri namba 2 Dar es Salaam.

Alisema baada ya Sheria ya Huduma ya Habari kupita kulikuwapo na malumbano makubwa kuwa sheria hiyo inakiuka sheria nyingi za kimataifa pamoja na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mkataba wa EAC.

Alisema waliona sehemu nzuri ya kufikisha shauri hilo ni kwa Mahakama ya Afrika Mashariki ambayo jana imetoa hukumu ikisema sheria hiyo inakiuka misingi ya haki za binadamu, utawala bora na yote ambayo yameainishwa katika kifungu cha 6 cha Mkataba wa EAC.

Alisema maamuzi ya mahakama hiyo yanaifunga nchi mwanachama kwa kuwa ni sehemu ya jumuiya, hivyo, Tanzania ina jukumu la kutekeleza maamuzi yaliyotolewa na mahakama hiyo.

Alisema maamuzi ya mahakama hiyo yanatekelezeka na kama hayatafanyiwa kazi basi watakuja tena mahakamani hapo kuomba utekelezaji wake.

## Kesi ya kina Mbowe

INATOKA UK. 7

Jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi na Wakili wa Serikali, Simon Wankyo, ulipinga hoja ya utetezi.

Nchimbi alidai kuwa mshtakiwa alitakiwa kuwasilisha taarifa kwa njia ya maandishi kuhusu kuridhia kesi kuendelea bila uwapo wake.

Hakimu alisema hoja za Jamhuri zina mashiko kesi hiyo itaanza kusikilizwa Aprili 17, mwaka huu na dhamana za washtakiwa zinaendelea.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni, Mbunge wa Tarime Mjini Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka huu, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam kwa kuwashawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Ilidaiwa Februari 16, mwaka huu Barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni, Wilaya ya Kinondoni kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya Ofisa wa Jeshi la Polisi, Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano wa hadhara mshtakiwa Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki kwa kutamka matamshi kwamba "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano... watu wanapotea...watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome..." alinukuliwa na kudaiwa kuwa maneno yaliyoelekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

Washtakiwa wote waliposomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.




## ... Afichua

INATOKA UK. 3

ya kodi ambayo mengi huwa feki.

Alisema wafanyabiashara wakubwa wana mashine za elektroniki zinazotumika kulipa kodi ya serikali, lakini hukwepa kodi kwa kuwa na mashine nyingine pembeni, hivyo malipo wanayotoa serikalini hayaendani na mauzo wanayoyafanya.

"Mkurugenzi Mkuu wa TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) aliwahi kunieleza kuwa kuna mtu aliingiza magari 192 bila ya kulipia kodi. Alikwepa kulipa kodi ya Sh. bilioni nane. Na huyo mtu anatetewa na watu, anawekewa kifua sana na watu," Rais Magufuli alisema.

Alibainisha kuwa kuna mkurugenzi ndani ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ambaye amewauzia wafanyakazi wa taasisi hiyo viwanja hewa vyenye thamani ya Sh. bilioni moja, lakini hajapelekwa mahakamani. "Wala sijapata taarifa kama hizo fedha amezirudisha kwa wafanyakazi, wafanyakazi wanaumia pembeni kwa kuwa aliyewatapeli ni bosi wao, amewadanganya kuwa ana viwanja eneo la Bagamoyo," Rais Magufuli alisema.

# JPM asimulia alivyofanikisha

INATOKA UK. 2

tunakuja nao wakashikwa," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema rushwa haina chama kwa kuwa hata ndani ya CCM kuna wala rushwa na aliwataka Takukuru kuhakikisha wanamkamata mtu yeyote anayejihusisha na vitendo vya kupokea na kutoa rushwa.

"Ukimkuta mwana CCM au Chadema anachukua rushwa mshike tu, kwa sababu rushwa ni ugonjwa. Rushwa ni tatizo katika nchi yetu, rushwa ndiyo mtindo wa maisha, ukienda ofisi fulani utaambiwa zangu ngapi au unatuachaje, kama rushwa itaisha au itapungua nchi hii itafanikiwa sana," alisema Rais Magufuli.

Maagizo kwa balozi Mlowola

Rais Magufuli alimtaka balozi Mlowola kwenda kutekeleza majukumu yake vizuri kwa kuwa Cuba ina mambo mengi yanayoweza kuisaidia Tanzania kama kilimo cha miwa na kuja kuwekeza viwanda vya sukari.

"Kitendo cha wewe kuwa balozi wa kwanza nchini Cuba nina imani nchi itanufaika sana. Wizara ya Mambo ya Nje itaendelea kusimamia matumizi mazuri ya balozi zetu," alisema Rais Magufuli.

HABARI KITAIFA

# Samia ataka uwekezaji sekta ya afya

**Na Devota Mwachang'a**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu, amesema kuwekeza katika sekta ya afya na teknolojia za kidigitali kutasaidia kutatua matatizo na changamoto za afya ya jamii kwa lengo la kufikia maendeleo endelevu.

Alibainisha hayo katika ufunguzi wa mkutano wa saba wa wanasayansi watafiti na watoa huduma za afya kutoka nchi tano za Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) jijini Dar es Salaam, ambapo pia alizindua mfumo wa teknolojia unaolenga kuboresha na kutatua changamoto za huduma za afya (Digital Health Technology).

"Kuwekeza katika sekta ya afya na teknolojia za digitali zinazofaa ni muhimu kwa maendeleo yetu ambayo tunahitaji kujiingiza kwa ukamilifu, sisi Tanzania tunahitaji kufanya zaidi katika sekta ya afya," alisema.

Alisema kuna uhitaji wa kufafanua na kutekeleza mipango ya mikakati ya afya ya kidigitali inayozingatia utaratibu wa utawala katika afya. "Changamoto yetu bado inabaki kwenye ukosefu wa nguvukazi ili kuunga mkono mipango ya Tehama na fedha za kuwafundisha wafanyakazi wapya na kuja na mipango mapya," alisema.

Makamu wa Rais alisema changamoto na suluhu zitabainishwa na kujadiliwa na washiriki wa mkutano, kisha zitawekwa katika maandishi kwa madhumuni ya kutumiwa na wakuu wa nchi husika za Afrika katika kuimarisha sekta ya afya.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema pamoja na uanzishwaji wa matumizi ya teknolojia nchini, bado kuna changamoto ya kukosekana kwa utayari wa watoa huduma za afya.

"Mfano Hospitali ya Taifa Muhimbili kupotea kwa mafaili kumepungua kwa asilimia 40-60 kutokana na matumizi ya teknolojia, tutaendelea kuhimiza watoa huduma watumie zaidi teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma za afya," alisema.

Waziri alisema wameona badala ya kutumia makaratasi katika hospitali kwa sasa kwa kuwa wananchi wengi wana simu, katika hospitali za serikali wanahakikisha zinatumia teknolojia katika utoaji wa huduma za afya ili kukabiliana na changamoto ikiwamo ya kupotea kwa mafaili.

Amewapongeza madaktari bingwa wa masuala ya uzazi na wanawake, Watanzania waliamua kuanzisha mtandao wa WhatsApp ambapo wanaoutumia.

Waziri wa Afya na Mapambano dhidi ya Ukimwi wa Burundi, Dk. Thaddee Ndikumana, alisema mradi huo utakuwa ni kitu muhimu kwa wananchi wa Afrika Mashariki, na kwamba Warundi wataweza kupata ushauri wa kitabibu kutoka Hospitali ya Muhimbili bila wao kuja. Naibu Katibu Mkuu EAC, Dk. Steven Mlote, alisema jumuiya hiyo ina wakazi zaidi ya milioni 170 na asilimia karibu 80 na zaidi wapo kwenye maeneo ya vijijini, ambayo hayafikiki kwa urahisi na usafiri ni shida na vituo vingi vya matibabu vipo mjini, hivyo teknolojia hii watafaidika nayo.



Msajili wa Tacip, Zinaida Said, akiwasajili wasanii wa sanaa na ufundi Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yataka ushirikiano na shule binafsi

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

SERIKALI imeahidi kuendeleza ushirikiano wake na shule binafsi kutokana na shule hizo kutoa mchango mkubwa katika sekta ya elimu.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Sekondari kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Benjamin Oganga, katika mahafali ya 14 ya kidato cha sita Shule ya Sekondari St. Mathew's Mkuranga mkoani Pwani. Oganga ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema serikali inatambua mchango ambao unafanywa na shule binafsi kwa kuwapatia elimu Watanzania wengi.

"Tunatambua mchango ambao unatolewa na shule binafsi kwa kuwapatia elimu Watanzania," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imepeleka walimu wake kufundisha katika baadhi ya shule binafsi, na kunapotokea mafunzo au mikutano ya elimu wamekuwa wakizialika shule binafsi kushiriki.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Christopher Segereti, aliiomba serikali iwasaidie mikopo wanafunzi wanaosoma shule binafsi.

Alisema wapo wanafunzi ambao waliosoma shule za serikali na wakakosa nafasi wakajiunga na shule binafsi, lakini inapofikia suala la mikopo wanakosa.

Pia alisema shule yao inaunga mkono jitihada za serikali, Tanzania ya viwanda, na kuwa asilimia 75 ya wanafunzi wanachukua masomo ya sayansi.

# TACIP wafika ukingoni Ubungo

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa utambuzi wa wasanii wa sanaa za ufundi Tanzania ujulikanao kama TACIP umefikia ukingoni wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, ikiwa ni wilaya ya pili baada ya Kinondoni kufikiwa na usajili wa mtaa kwa mtaa tangu zoezi la utambuzi wa mradi huo uanze.

TACIP inaendeshwa kwa ubia kati ya kampuni ya DataVision International na Shirikisho la Sanaa Tanzania (TAFCA ) na kusimamiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

Mlezi Mkuu wa mradi akiwa ni Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, na unalenga kuwafikia wasanii wote wa sanaa za ufundi nchini.

Kwa Wilaya ya Ubungo utafikia tamati mwisho wa wiki hii, ukiwa umefanikiwa kupata taarifa na kusajili wasanii zaidi ya 2,000.

Akizungumza wakati wa zoezi la usajili likiendelea, Mratibu wa TACIP, Sauli Mpock, aliishukuru serikali akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, watendaji kata na mitaa, wajumbe wa wilaya hiyo pamoja na wasanii wote waliojitokeza kujisajili.

"Tunashukuru sana kwa mapokeo tuliyoyapata wilayani hapa kwa kuwa wasanii wengi wa wilaya hii wameonyesha kuvutiwa na mradi huu zaidi. Vilevile ningependa kutoa wito kwa wasanii wengine wa wilaya zilizobaki kama Temeke, Ilala na Kigamboni kuupokea na kujitokeza kwa wingi kujisajili kwani mradi huu utarudishia heshima na thamani ya wasanii kwa kuwezesha kutambulika na mamlaka ya ndani na nje ya nchi," alisema.

Ofisa Utamaduni na Michezo wa Wilaya ya Ubungo, Fredy Kadewele, aliupongeza mradi huo na kufurahishwa na fursa hiyo kwa wasanii wa wilaya hiyo. "Tumefurahia sana mradi huu kwa kuwa unatoa fursa kwa wasanii wa wilaya yetu sio tu katika kutatua changamoto zinazowakabili bali katika kuboroshe sanaa ya ufundi kwa ujumla na ninadiriki kusema TACIP ni mkombozi wa sanaa ya ufundi Tanzania," alisema Kadewele.

# Waomba askari kudhibiti tembo

Na Beatrice Shayo, RUFIJI

WANANCHI wa Kijiji cha Mloka Tarafa ya Mkongo wilayani Rufiji, wameiomba serikali iwasaidie kuwapatia askari wa wanyamapori ili kusaidia kuwaondoa tembo wanaovamia mazao yao.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kwa niaba ya wananchi wenzake, Asia Selemani, alisema kijijini hapo hawana askari wa wanyamapori wa kudhibiti wanyama hao. Alisema kwa sasa tembo ni wengi na wanapokuwa wanavamia mazao yao wanashindwa kuwafukuza kwa sababu hawana uelewa na kuogopa kuhatarisha usalama wa maisha yao.

"Tungepatiwa askari wa wanyamapori hapa kijijini ili watusaidie katika kuwaondoa hao tembo wanapovamia mazao yetu, maana tembo akivamia shamba mfano lenye mpunga hatoki, huwa tunajaribu kuwafukuza hawataki kuondoka, hivyo tungepatiwa hao wataalamu wangetusaidia," alisema Selemani.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mloka, Ahmed Mloya, alisema kijiji hicho kipo karibu na pori la Akiba la Selous na kwa sasa kumekuwa na changamoto ya wanyama kuingia katika mazao akiwamo tembo. Alisema hali hiyo imetokana na ongezeko la wanyama katika hifadhi hiyo, kwa kuwa awali walikuwa hawaonekani ikilinganishwa na sasa.

Alisema kuonekana kwa wanyama hao kwa wingi ni jitihada za serikali za kupambana na ujangili. Alisema wanafurahia kuongezeka kwa wanyama na wananchi kwa sasa wanashirikishwa katika uhifadhi wanyamapori hali ambayo imesaidia katika kutatua tatizo la ujangili.

Alisema wananchi ambao walikuwa wanadaiwa kuhusika na ujangili wameacha na kuwasilisha silaha zao na kwa sasa wanaelewa umuhimu wa uhifadhi wa wanyamapori.

"Kijiji chetu kilipatiwa ufadhili wa kusomesha vijana skauti hawa wanatusaidia katika kupambana na ujangili na wanapoona kuna jambo ambalo sio zuri wanatupatia taarifa na kulifanyia kazi," alisema.

Mloya alisema maendeleo makubwa yanaletwa na utalii na ndio maana wameamua kusimamia raia wasio wema kuacha vitendo vya ujangili.



Kazi ya ujenzi wa barabara ikiendelea Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam juzi. Hata hivyo, wafanyabiashara wadogo wa eneo hilo wamekuwa wakikumbana na changamoto ya kuhamishwa kupisha ujenzi huo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Lindi yahimizwa kutenga maeneo ujenzi viwanda

Na Mwandishi Wetu, LINDI

MAMLAKA ya Ukanda Maalum ya Uwekezaji nchini (EPZA), imeuhimiza Mkoa wa Lindi kukamilisha mchakato wa kutenga na kuandaa maeneo ya uwekezaji wa viwanda kama kivutio muhimu cha wawekezaji wa ndani na nje.

Hayo yalisemwa jana mkoani hapa na mwakilishi wa EPZA, Grace Lemunge, katika kilele cha Jukwaa la Biashara.

"Kama taasisi ya uhamasishaji wa uwekezaji wa viwanda vya uzalishaji kwa mauzo ya nje tunatoa wito kwa Mkoa wa Lindi kumalizia mchakato wa kutenga na kuandaa maeneo ya uwekezaji wa viwanda, kwa kuwa ardhi ndiyo siri kubwa ya mafanikio katika sekta ya viwanda," alisema Lemunge alipokuwa akitoa mada katika Jukwaa la Biashara na Uwekezaji mkoani Lindi.

Lemunge aliongeza kuwa nchi mbalimbali ziligundua siri ya kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda na ndiyo sababu zikaweza kupiga hatua kwenye sekta ya viwanda, hivyo ameutaka Mkoa wa Lindi kutimiza azima ya serikali ya kufikia Tanzania ya viwanda kwa kuwa na eneo ambalo linaweza kuwa suluhisho katika kutimiza dhana ya Tanzania ya Viwanda.

Alisema kutenga maeneo ya viwanda ukifanikiwa na viwanda kujengwa kwa wingi, itasaidia uboreshaji wa uchumi ambao utasababisha uzalishaji wa bidhaa kuongezeka na kuleta manufaa makubwa katika uchumi wa taifa.

Ujenzi wa viwanda vingi kutaiwezesha nchi kupata fedha za kigeni, ambapo uzalishaji ukiongeza itasababisha uuzwaji wa bidhaa nje ya nchi kuongezeka, hivyo nchi kunufaika na pato la fedha za kigeni, katika ustawi wa shilingi ya Tanzania.

Lemunge aliongeza kuwa usindikaji wa malighafi za ndani utapunguza uuzaji nje bidhaa ghafi hali ambayo haikubaliki katika dunia ya sasa, hivyo lazima hatua zichukuliwe za uhamasishaji usindikaji wa malighafi ili kuongeza thamani, hivyo kupata faida zaidi.

"Utengaji wa maeneo kwa ajili ya viwanda utarahisisha wawekezaji kupatikana kwa kuwa wapo ambao wana teknolojia mpya ambazo hazipatikani nchini, hivyo kutasaidia Watanzania kujifunza na kuzitumia," alisema.

# Serikali yawapa jukumu wabunifu

Na Elizabeth Zaya

SERIKALI imewataka wabunifu nchini kubuni teknolojia zinazoendana na mazingira halisi ya nchi na ambazo si za kujifurahisha, zinazoweza kufanya kazi katika kipindi hiki cha ujenzi wa Tanzania ya Viwanda.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, wakati akizindua Wiki ya Ubunifu jijini Dar es Salaam.

"Kwa nchi yoyote ambayo inaendelea, hauwezi kuendelea, kiendelevu kama hauna teknolojia ambayo inatoka kwako, ambayo inaendana na mazingira halisi ya nchi yako. Kwa hiyo ndiyo maana tunataka Watanzania wawe wabunifu, waweze kubuni bidhaa na teknolojia ambazo zitatusaidia kama nchi," alisema Ole Nasha na kuongeza:

"Na ndio maana tunajaribu kuwasaidia wabunifu wetu ili mawazo yao ya ubunifu yaende kwenye hatua ya kuanza kutumika kama bidhaa sokoni. Kuwa na wazo ni kitu kingine, lakini kama huwezi kuliendeleza na kutengeneza bidhaa au huduma inakuwa haina maana."

Alisema serikali imeanzisha mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ambayo yanatoa fursa kwa wabunifu kuonyesha ubunifu wao na kwamba baada ya mashindano huchukua washindi na kufadhili kazi zao kwa kuzipeleka katika hatua ya kuziendeleza na kuzitengeneza kwa ajili ya matumizi.

"Na ndiyo maana pia tunatumia wiki hii kusaidia kuwaleta wabunifu mbalimbali kuonyesha kazi yao, lengo ni kuona namna gani wanaweza kusaidiwa ili ziweze kutumika," alisema Ole Nasha.

Alisema katika kuweka mazingira bora ya ubunifu, serikali imeanza mchakato wa kuboresha Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambayo imepitwa na wakati.

"Sayansi, teknolojia na ubunifu ni vitu ambavyo vinabadilika kwa haraka sana, sera yetu tumeibadilisha ili iendane na mazingira ya sasa, lakini ituongoze namna ya kuwatambua wabunifu na kuendeleza kazi zao, tumefika hatua nzuri na hivi karibuni tunatarajia kwamba itafika katika Baraza la Mawaziri na hatimaye kupitishwa kwa matumizi," alisema Ole Nasha.

Wiki ya Ubunifu nchini imeandaliwa na Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF) na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa ufadhili wa wa serikali ya Uingereza kupitia Shirika la UKaid.



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akifungua Kikao cha Tano cha Kamati ya Demokrasia na Utawala cha Baraza la Wabunge wa Mabunge ya Jumuiya ya nchi za Maziwa Makuu (FP-ICGLR) jijini Arusha jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Aliyedaiwa kutekwa Namanga Kenya apatikana akiwa salama

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

RAIA wa Kenya aliyedaiwa kutekwa juzi na kusababisha taharuki kubwa katika eneo la mpaka wa Namanga wa Tanzania na Kenya amepatikana akiwa salama hatua ambayo imerejesha utulivu katika eneo hilo.

Akizungumzia tukio hilo, Ndutu Keruu mkazi wa Namanga upande wa Kenya, alidai gari lililokuwa na namba za Tanzania likiwa na watu waliovaa kiraia, walifika kwenye duka la raia huo wa Kenya maarufu kwa jina la Moha na kumuamuru afunge biashara na kisha wakaondoka naye kusikojulikana.

"Wakati wakimlazimisha kupanda gari, Moha alionyesha ujeuli kwa kuwa akidai watu hao hawana mamlaka ya kumkamata," alisema.

Alisema baada ya Moha kukataa raia waliokuwa jirani na duka hilo walilizingira gari hilo, wakizuia Moha kuchukuliwa.

"Walituuliza kwanini tunawazuia kumchua mtu wao, na baada ya muda mfupi zikasikika sauti za milio ya risasi na hivyo watu wakakimbia na Moha akachuliwa.

"Hali ile ilitushangaza sana, tukaamua jana (juzi) kufunga mpaka huu wa Namanga kwa kuchoma matairi hadi hapo Moha atakapo patikana.

"Kama Moha ni mhalifu, wangewasiliana na polisi wa Kenya ili wamkamate na wa mkabidhi kwa mamlaka husika, lakini si wao kuja kwetu kukamata raia, bora hata wangekuwa wale polisi wa kimataifa (Interpol) wamefanya hivyo maana hawana mipaka," alidai.

Mkazi mwingine wa Namanga upande wa Kenya, John Njoroge, naye alidai chanzo cha polisi wa Tanzania kuja kumchukua Moha, ni kwa sababu alionekana kumtapeli mmoja wa wananchi wa Tanzania kwa kumbadilishia fedha na kumkata kiasi kikubwa.

"Alikuja raia wa Tanzania kubadili fedha ili apatiwe ya Kenya, sasa Moha alimdhulumu, yule raia alivyoenda upande wa nchi yake akagundua amedhulumiwa ndipo akatoa taarifa kwa polisi na polisi wakamfuatilia na wakati Moha akichukuliwa yule raia naye alikuwa kwenye hiyo gari," alidai Njoroge.

Alisema haiwezekani polisi wa Tanzania kuingia bila kuwasiliana na polisi wa Kenya, wamewasiliana na hata kwenye gari kulikuwa na polisi wa Kenya lakini yeye hakushuka kwenye gari wakati Moha anachukuliwa.

"Haiwezekani risasi ifyatuliwe halafu polisi wa Kenya wakae kimya, walikuwa na taarifa ya kilichokuwa kinaendelea," alidai Njoroge.

Lakini pia Moha si mara ya kwanza kubadilishia watu fedha na kuwadhulumu, na hata ile fujo jana imefanyika hapa mpakani ni Wasomali wamefanya (Oria).

"Wasomali sasa wanataka kugeuza nchi yetu ni ya kwao, hii si mara ya kwanza wao kufanya fujo, tena wamewanunulia pombe hawa wala mirungi ili wafanye fujo, hatutaki huu ujinga kwetu," alisema Njoroge.

Akilalamikia kitendo cha wajasiriamali kufungwa maduka yao na abiria kushindwa kusafiri kuwa kimewaathiri vikubwa kiuchumi.

"Sisi raia wa Kenya hatuna shida wala chuki na Watanzania, sisi ni wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, sisi ni ndugu, tusichonganishwe, tufanya kazi kwa ushirikiano," alisema.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alithibitisha kupatikana kwa raia huyo wa Kenya na alisema tayari amekabidhiwa kwa polisi wa Kenya.

"Hatuna uhakika kama alichukuliwa na polisi wetu, kwa sababu hawana ushahidi wowote unaoashiria kuwa alitekwa na polisi wa Tanzania, hapa ni mpakani kuna matukio mengi sana ila ameshapatikana," alisema.

Alisema wananchi wa Kenya walifunga barabara na kuchoma moto matairi pamoja na kuharibu jengo la EAC kwa kuvunja vioo na kuharibu vifaa vya ofisini.

"Hakuna athari ya kifo kwa watu wangu, zaidi ni biashara zilikwama tu kutokana na vurugu hizo," alisema Mwaisumbe.

"Kwa sasa hali ni shwari katika mpaka wa Namanga na magari yameanza kutoka na kuingia nchi zote mbili, biashara zinaendelea kama kawaida.

"Niwatake wananchi kuondoa hofu mpaka wetu upo salama, endeleeni na majukumu ya kujenga taifa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema hana taarifa za mtu yeyote kutekwa na polisi au rai wa Tanzania.

"Sina hizo taarifa, ninachojua ni Wakenya wamechoma matairi barabarani na kuzuia magari yasiingie nchini mwao," alidai.

Alisema baada ya kupata taarifa za vurugu hizo, alifika eneo hilo kuhakikisha watu wake wanakuwa salama, hivyo hali ni shwari watu wanaendelea na majukumu kama kawaida.

"Kama mfanyabiashara wa Kenya katekwa, hilo ni suala la Wakenya wenyewe halipo kwetu, sijui kama amepatikana au hajapatikana na sina taarifa za aina hiyo ni ushauri jaribu kupata mawasiliano na viongozi wa Kenya ila mimi sina hayo majibu wala taarifa," alidai.

Nimalizie kwa kusema ukiona kwa jirani kunawaka moto, wahi kudhibiti usifike kwako, hivyo mimi nimehakikisha Namanga-Tanzania hali ni shwari.

# Japan yamwaga mil.195/- ujenzi madarasa

**Na Allan Isack,** ARUMERU

UBALOZI wa Japan nchini, umeingia makubaliano na Halmashauri ya Arusha DC, kutoa fedha kiasi cha dola za kimarekani 87,974, sawa na Sh. milioni 195, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa lenye madarasa manne katika Shule ya Sekondari ya Sokon II.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kusaini mkataba wa ujenzi wa jengo hilo, na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Balozi wa Japan hapa nchini, Shinishi Goto, alisema kuwa nchi hiyo, imefikia hatua ya kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo, kwa lengo la kuunga mkono sera ya serikali ya elimu bila malipo.

Alisema kuwa serikali ya Japan imetoa fedha kiasi cha dola za kimarekani 87,974, sawa na shilingi milioni 195, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne kwa mfumo wa ghorofa katika Shule ya Sekondari ya Sokon II.

Aliongeza kuwa katika ujenzi huo, utaambatanishwa pamoja na kuwekewa vifaa vya thamani kwa madarasa yote manne.

Balozi huyo, alisema kuwa, Serikali ya Japan inashirikiana vyema na Serikali ya Tanzania, na imeona kuna umuhimu wa kuunga mkono mpango wa sera ya elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, alifafanua kuwa, kiasi hicho cha fedha, kilichotolewa na ubalozi wa Japan, kitawezesha ujenzi wa msingi wa ghorofa hilo, lenye vyumba 12 vya madarasa, lakini kiasi hicho, kitaweza kukamilisha vyumba vinne vya madarasa, pamoja na kuviwekea thamani.

Mahera, aliongeza kuwa hadi kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo kwenye shule hiyo kuna uhitaji wa kiasi cha fedha Sh. milioni 330.2 .

Aidha, aliongeza kuwa kiasi cha Sh. milioni 90, kitatolewa na serikali kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, na fedha nyingine kiasi cha Sh. milioni 50, zitatolewa na halmashauri hiyo kupitia mapato yake ya ndani.

"Hadi kukamilisha kwa jengo hili lenye vyumba 12 vya madarasa tunahitaji Sh. milioni 330.2, hivyo serikali itashirikiana na ubalozi wa Japan kukamilisha ujenzi wa mradi huu, ambao madarasa haya yakikamilika tutakuwa tumemaliza kabisa tatizo la uhaba wa madarasa kwenye shule hii," alisema Mahera.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Sokon II, Mwamvita Kilonzo, alithibitisha kuwapo kwa changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa shuleni hapo, ulio wiana na idadi kubwa ya wanafunzi waliosajiliwa shuleni hapo.

Aliongeza kuwa shule hiyo, ina jumla ya wanafunzi 1,006, ikiwa na vyumba 11 vya madarasa na kuna uhitaji wa vyumba vingine 11, ili kufikia vyumba 22, ambavyo vitawiana na idadi ya wanafunzi.

Mhandisi wa ujenzi wa halmashauri hiyo, Bibie Manzi, alisema kuwa utekelezaji wa mradi huo, uko katika hatua za awali na mchakato wa kumpata mkandarasi wameshakamilisha, hivyo wanatarajia ujenzi mwezi ujao na kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.





# ‘Mateja’ wageukia kuvuta sumu ya panya kama kilevi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BAADA ya vita ya kupambana na dawa za kulevya kushika kasi kila kona nchini na kusababisha kupungua kwa mihadarati sokoni, watumiaji wa dawa hizo maarufu kama ‘mateja’ wameibuka na ulevi mbadala wa kutumia sumu ya panya.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema asilimia kubwa ya vijana kwa sasa wanatumia dawa za kulevya zenye kemikali za sumu kutokana na serikali kuthibiti uingizwaji wa dawa hizo.

Waziri huyo amekiri kuibuka kwa tatizo hilo la matumizi ya sumu ya panya kama kilevi mbadala, wakati alipokuwa akizungumza na vijana wa skauti wa Mkoa wa Kilimanjaro.

“Asilimia kubwa ya vijana kwa sasa wamebainika kutumia kemikali za sumu baada ya serikali kudhibiti biashara ya dawa za kulevya kwa asilimia 90. Sasa wamebuni mbinu nyingine mpya ya kutumia sumu ya panya na dawa za usingizi kama mbadala wa dawa za kulevya,” alisema waziri huyo.

Kwa mujibu wa Waziri Mhagama, asilimia 56 ya nguvu kazi hapa nchini ni vijana na kwamba kama hatua za kudhibiti kundi hilo kubwa lisiendelee kuathiriwa na dawa za kulevya kuelekea uchumi wa kati wa viwanda halitapewa msukumo zaidi, kuna hatari ya kukosa vijana watakaokuwa na uwezo wa kufanya kazi.

Awali, Kamishna wa Skauti Mkoa wa Kilimanjaro, Brighton Matola, akizungumza kuhusu hali hiyo alisema vijana wengi kwa sasa wanatumia dawa mbadala kuvuta na kujidunga, hali ambayo imekuwa ni changamoto kubwa kuwadhibiti. Alisema wanachofanya kwa sasa ni kuendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya.

“Kuna changamoto kubwa sana kwa vijana katika uraibu wa dawa za kulevya kwa vijana, ambapo skauti wamejitahidi kupambana na matumizi hayo, lakini changamoto ni hii ya kuibuka tena matumizi mbadala ya dawa hizo pamoja na unywaji wa pombe uliopindukia. Watumiaji wa dawa nyingi wamekuwa wakitumia kwa kuvuta na kujidunga,” alieleza Matola.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Dk. Japhet Boniface, alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu madhara na aina ya wagonjwa wanaofikishwa hospitalini hapo, alisema dawa za kulevya zimekuwa na athari kubwa kwa vijana, baada ya kuvuta kemikali hizo husababisha ubongo kupata madhara pamoja na miili yao kudhoofu na hivyo kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

“Watumiaji wa mihadarati nchini Tanzania, wamegeukia dawa za usingizi kama njia mbadala baada ya kuadimika kwa dawa za kulevya. Wakati wengine wakidaiwa kuonekana kukimbilia katika vituo vya kutunza mateja au nyumba za matibabu, wanalazimika kutumia vileo mbadala ili kukidhi haja ya miili yao,” alisema.

Katika miaka ya hivi karibuni, serikali ya Tanzania imeweka mkakatai madhubuti kukabiliana na dawa za kulevya na matokeo yake ni kupungua kwa uingizwaji wa mihadarati kama heroine na cocaine.

Baadhi ya waraibu wa mihadarati, maarufu kwa jina la mtaani kama mateja, wamejisalimisha hospitali kupata msaada wa kitabibu ili kuachana na matumizi ya dawa hizo.



Wabeba mizigo katika Soko la Feri jijini Dar es Salaam, wakipokea vikapu vya samaki kwa ajili ya kupeleka mnadani katika soko hilo.
**PICHA: HALIMA KAMBI**

# Mkurugenzi afagilia wasaidizi wa kisheria

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

UAMUZI wa serikali wa kuhamasishwa jamii kuwatumia wasaidizi wa kisheria kutatua matatizo yao na kupata ushauri baada ya kuhisi haki zao zimechezewa, umesaidia kuleta mabadiliko kwa taifa na vizazi vijavyo katika sekta za uchumi, jamii, siasa na elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, amesema wasaidizi wa kisheria ni sehemu ya mpango na mkakati wa serikali kuhakikisha kuwa inafikia uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

“Kwa uwezo wao na namna navyoona wanavyojituma katika baadhi ya maeneo licha ya uchache wao na kukosa bajeti ya kukabiliana na matatizo yanayoikabili jamii humo mitaani, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, sisi tutatoa ushirikiano na tayari tumeshaunda kamati maalum ya kusaidia hilo,” alisema.

Kauli ya Lubuva inakinzana na mtazamo wa Jaina Mwena ambaye ni mmoja wa wasaidizi wa kisheria wilayani humo, ambaye ameeleza kutoridhishwa kwake na mwitikio hafifu wa baadhi ya viongozi wa serikali na mawakili kukubaliana na huduma inayotolewa maeneo ya vijijini na mjini.

“Kuwatumia wasaidizi wa sheria kuna punguza muda unaotumika mahakamani, nadhani wananchi wengi wasio na uwezo wanalazimika zaidi kutumia fursa hii waliyopewa na sheria kupata msaada wa kisheria kupitia wananchi wenzao waliojitolea kwa moyo kutoa ushauri na kimsingi sisi hatuingii kwenye migogoro au mambo yanayoonekana ni jinai,” alisema Mwena.

Alisema licha ya wananchi wachache kutambua huduma hiyo ipo na inatolewa kwa mujibu wa sheria, bado yapo mambo mengi ambayo ni tatizo katika Wilaya ya Mwanga na wamepanga kuyashughulikia.

Changamoto hizo ni pamoja na wakati mwingine kutoheshimiwa kwa haki za binadamu, ukatili dhidi ya watoto kama kunyimwa haki ya elimu, chakula, elimu, huduma za afya na kuishi na wazazi.

Aidha, msaidizi huyo wa kisheria ameeleza masikitiko yake kuhusu urasimu unavyolitikisa zoezi la usajili wa wasaidizi wa kisheria katika baadhi ya maeneo na kushauri wanaotengeneza ugumu huo kutambua wanahitajika zaidi katika jamii kuliko kitu kingine kwa sasa.

Sheria ya Huduma ya Msaada wa Sheria ya Mwaka 2017 na kanuni zake za mwaka 2018, kanuni ya 10 inayozungumzia uamuzi kuhusiana na maombi ya wasaidizi wa sheria inaeleza bayana msajili baada ya kujiridhisha na maombi na viambatisho vinavyotakiwa kwa ajili ya usajili, atamsajili msaidizi wa kisheria kama mtoa huduma ya msaada wa kisheria na atampatia cheti cha usajili kama kilivyobainishwa katika jedwali la saba la kanuni.

# DC ataka taasisi za umma kuacha urasimu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imezitaka taasisi za umma zinazogusa moja kwa moja mahitaji ya sekta ya uwekezaji kuacha urasimu badala yake ziweke ushirikiano wa pamoja ili kuondoa vikwazo visivyo vya lazima ambavyo vinachangia kuwakatisha tamaa wawekezaji wanaokuja kuwekeza nchini.

Hayo yamo katika hotuba ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliyoitoa jana, wakati akifungua kikao kazi cha taasisi za umma kinachozijumuisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Mamlaka ya Mapato (TRA), Shirika la Ugavi Umeme (Tanesco), Uhamiaji, Idara ya Kazi, Ardhi na Maofisa Biashara.

“Mkiacha ule urasimu wenu mnaotaka kunyenyekewa ili kutimiza wajibu wenu ambao uko kisheria, suala la vikwazo au mwekezaji kulalamikia hili na lile mtakapotoa ushirikiano sekta ya uwekezaji itakuwa na mchango mkubwa kwa taifa. Urasimu hauna nafasi katika serikali hii, tuhakikishe wawekezaji wanapata mahitaji ya msingi ili wawekeze mitaji yao,” aliagiza.

Badala yake, Warioba ametoa wito kwa taasisi hizo za umma kuishauri serikali pale inapoonekana kusababisha vikwazo katika utekelezaji wa baadhi ya masuala ambayo hayatengenezi mazingira rafiki katika kukuza sekta ya uwekezaji nchini.

Kikao hicho kiliandaliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC) cha Mkoa wa Kilimanjaro, kwa ajili ya kuwekana sawa kutekeleza majukumu yao na kuweka mpango mkakati wa kuvutia uwekezaji.

Mkoa wa Kilimanjaro unaufuata Pwani kwa kupata miradi mingi inayochangiwa na miundombinu bora na mazingira rafiki kwa wawekezaji wakubwa na wadogo.

Katika kikao hicho, Meneja wa TIC Kanda ya Kaskazini, Daudi Riganda, alisema taasisi hizo zitaunda kamati ya kusimamia uwekezaji mkoani Kilimanjaro, lakini pia zitafanyika vikao vingine katika mikoa ya Arusha, Tanga na Manyara ili kuwaondolea vikwazo wawekezaji.

Alisema kamati hiyo itakuwa na jukumu la kurahisisha huduma kwa wawekezaji, ingawa aliongeza kuwa hali ya uwekezaji mkoani hapa ni ya kuridhisha licha ya kuwa na changamoto ndogo zinazoshughulikiwa na ofisi za Uhamiaji, Idara ya Kazi na nyinginezo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Uhamiaji mkoani hapo, Albert Rwelamira, alitoa wito kwa wawekezaji wa kigeni kufuata sheria ikiwamo kutofika nchini na kuanza kazi kabla ya kukamilisha kwa taratibu za kuwa na vibali vya kufanyakazi.



## Umemejua Korogwe ulivyowapaisha kinamama kuelekea maisha mbadala

Ukurasa 14

BIASHARA



## Kagame ang'aka namna Afrika inavyojimaliza kupitia biashara

Ukurasa 19

# BUFE

ijumaa MACHI 29, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Ulemavu ghafla ulimgeuza mjamzito tegemezi, sasa anahudumia kundi

Ukurasa 16

UCHUMI ZAIDI Ukurasa 18

Takwimu za Uchumi Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Biashara**

**KIELEZO**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,477.39 | -4.11 |
| DSEI | 2,066.89 | -2.11 |

Thamani za Hisa

| | |
|---|---|
| (bln) | 19,922.46 |
| Mauzo | 163,344,640.00 |
| Hisa | 1,024,036 |

**ZILIZOPANDA**

| kAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| USL | 15 | +50.00% |
| ACA | 6,150 | +0.82% |
| JHL | 9,600 | +1.05% |

**ZILIZOSHUKA**

| | | |
|---|---|---|
| SWIS | 1,700 | -15.00% |
| EABL | 4,660 | -0.43% |
| KA | 115 | -4.17% |

# UCHUMI


**Na Jenifer Julius, aliyekuwa**
KOROGWE

# ILIKO NISHAT

## Umemejua Korogwe ulivyo kinamama kuelekea maish



Kinamama wa kijijini Mpale, Korogwe wakiwa sokoni. Kwa sasa ni wahitaji wakubwa wa huduma rasmi ya umeme. **PICHA: JENIFER JULIUS**.




Takwimu inay rogwe 2016/2

NUSRA Ibrahim, mkazi wa kijiji cha Mpale, katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, ameamua kutumia fursa ya umemejua kujiongezea kipato. Mwanamke huyo mwenye mume na watoto wawili, alianza kuuza mgahawa mwaka 2015 akitoa huduma ya chakula kuanzia chai nyakati za asubuhi hadi chakula cha mchana.

Sababu za zinazomfanya Nursa kutofanya biashara yake usiku, ni kukosekana mwanga wa uhakika kutokana na kibatari kutokuwa nishati ya taa rafiki.

Ulipoingia umeme mwaka 2017, alikuwa mmoja wa wateja wa mwanzo kuunganisha umeme katika mgahawa wake siyo tu kwa ajili ya ufahari bali ni sehemu ya mikakati ya kukuza biashara yake.

Umeme kwake ulikuwa zaidi ya huduma.

**Maisha mapya**

Akiwa na uso uliojaa tabasamu wakati akihudumia wateja kwenye mgahawa wake ulio katika hali ya usafi wakati wote, Nursa anasema kwa sasa ana majokofu mawili, moja ni maalum kuweka soda na nyingine maji, askirimu na maji ya kufunga kwa ajili ya wateja wanafunzi.

Anataja faida anayoipata katika biashara yake, inamsaidia kushirikiana na mume wake kuhudumia familia na sasa wamefanikiwa kujenga nyumba moja.

Nusra ni mmoja wa wanawake mkoani Tanga, wanaopambana kusaka kipato kuhudumia familia na kujikwamua kiuchumi, lakini kutokana na upungufu wa huduma za kijamii walijikuta wakishindwa kufikia malengo yao.

Hali kadhalika kati ya kaya 67,129 zinazomilikiwa na wanawake vijijini mkoani Tanga, asilimia 71.1 zinakiri umeme unawaongezea muda wa kufanya kazi usiku.

Hilo linathibitika kijijini Mpale, ambako Nipashe imeshuhudia shughuli nyingi za kuongeza kipato zikifanywa na kinamama, hasa nyakati za usiku.

Mwajuma Khamisi, anayeuza kalmati, maandazi, bajia na keki, sasa anafanya kazi hadi saa tatu usiku akikanda unga na anaamka saa nane usiku kupika ili kuwahisha biashara yake sokoni.

Kabla ya kuwapo umeme kijijini hapo, Mwajuma anasema alilazimika kuandaa biashara yake asubuhi wakati kumepambazuka, kwani mazingira ya giza hayakuwa rafiki kwa ufanyaji shughuli zake.

"Nilikuwa nasubiri kupambazuke, ndio nipike kwa sababu mwanga wa kibatari hautoshelezi, pia si salama kwa afya," anasimulia Mwajuma na kuongeza:

"Sasa napeleka vitu eneo la kuuzia mapema tofauti na zamani, nilikuwa nakuta wenzangu wenye biashara moja wameshamaliza kuuza. Kwa sasa kwa

> **"Katika kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini wananufaika na nishati sawa na wale wa mijini, tunatengeneza kikokotoo ambacho kitapima na kudhibiti gharama za juu za nishati, ili kudhibiti bei zinazowekwa na wawekezaji wa umeme."**

siku napata faida ya wastani wa Sh. 15,000 wakati zamani nilikuwa napata 8,000."

Katika kuhakikisha kuwa nishati hiyo inatumika kuleta maendeleo ipasavyo, baadhi ya wanaume wamejitoa kuwanunulia wake zao vifaa vya kufanyia biashara ili kukuza kipato cha familia.

Zephania Abdallah, anasema baada ya kuweka umeme nyumbani kwake, mume wake amenunua friji na sasa anauza barafu na maji ya baridi.

Anasema kutokana na wingi wa majukumu walio nayo, mumewe sasa anamsaidia majukumu mbalimbali, ikiwamo kufunga maji.

Mume huyo aitwaye Steven George, anasema aliamua kununua jokofu hilo ili kumsaidia mke wake katika biashara hiyo yenye tija katika familia yao.

"Kwa kuwa uhitaji wa maji na barafu ni mkubwa inabidi nimsaidie mwenzangu. Tunafunga maji vifuko 200 na barafu vifuko 100 na kipindi cha jua huwa vinaisha vyote kwa siku," anaeleza Steven.

Tangu wapate umeme kupitia mradi wa umemejua kijijini hapa, wanawake wamehamasika. Sasa hivi kila nyumba yenye umeme mwanamke anafanya biashara.

Augustine Mganga, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa kijiji cha Mpale, anasema umeme umeongeza fursa za kiuchumi kwa kinamama katika eneo hilo.

"Hata vikundi vya maendeleo ya kinamama (vicoba) vimejaa sasa, kabla ya umeme kuwapo wengi walikuwa wapo tu nyumbani wakihudumia familia na kilimo," anasema Augustine.

**Msimamizi Miradi**

Jafari Muhidini, ni Msimamizi wa Mradi wa Umemejua, katika kijiji cha Mpale, anaeleza kuwa wanawake wamekuwa ndiyo wateja waaminifu zaidi tangu kuanzishwa mradi huo.

Anasema kati ya kaya 156 walizounganishia umeme, nyingi zimetokana na hamasa kwa wanawake.

"Hata katika ulipaji wa madeni wanawake katika kijiji hiki wapo mbele na wanatupa moyo wa kuendelea kuwapo hapa. Wakati mwingine wanakuja kulipia madeni ya waume zao, ili mradi tu umeme usikatwe waendelee kuutumia," anasema Jafari.

Pamoja na mafanikio wanayoyapata kutokana na uwapo wa umemejua katika kijiji hicho, wanawake wanalalamikia gharama kubwa za umeme huo kuwa kikwazo cha mafanikio zaidi.

**Kilio cha gharama**

Rehema Athuman, anasema licha ya kunufaika na umeme kwa matumizi ya nyumbani kama vile taa, kuchaji simu na kusikiliza redio, bado hafurahii kutokana na gharama kubwa zlizopo.

Anasema analazimika kulipia



UCHUMI

**Ulemavu ghafla ulimgeuza mjamzito tegemezi, sasa anahudumia kundi**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Wajipanga kukagua uchumi wa miaka 25 kutoka safari Beijing**


Ukurasa 18

BIASHARA

**Kagame ang'aka namna Afrika inavyojimaliza kupitia biashara**

Ukurasa 19

# TI JUA
# owapaisha
# a mbadala




imu Hali ya Upatikanaji wa Nishati mwaka 2016/2017 Mchoro:Jenifer Julius

oonyesha hali ya usambazaji umeme, kijini Mpale, Ko-
017.



Viongozi wa Serikali ya Kijiji cha Mpale wakiwa ofisini kwao **PICHA: JENIFER JULIUS**

wastani wa Sh.33,000 kwa mwezi, Sh.11, 000 ikiwa ni gharama za umeme na Sh. 22,000 ni gharama za kuunganishiwa umeme.

Mama huyo anasema, kuna wakati huduma za kijamii zinapotolewa kwa gharama kuwa husababisha baaadhi ya wanawake kutochangamkia fursa, hivyo wanazidi kudidimia kimaendeleo.

Zariana Abdu anasema haoni haja ya kuweka umeme nyumbani kwake, kwa sababu anasikia wenzake wanalalamika gharama kubwa zaidi, jambo linalomfanya asinufaike na nishati hiyo kwa idadi ya wateja kupungua .

Umeme wanaotumia kina mama hawa ni matokeo ya umeme wa gridi ndogo ya umeme jua iliyofungwa kijijini na mwekezaji binafsi Ensol, kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine wa maendeleo.

**Wenye umeme**

Katika ufafanuzi wake kuhusiana na malalamiko ya gharama, Prosper Magali, Mkurugenzi wa Miradi kutoka Ensol, anatetea tozo lao kwamba ni dogo, akidai kuwa kwa mwezi ni Sh.11000, ambayo inawapa fursa watumiaji kujinufaisha kwa mengi, hasa matumizi ya kibiashara.

Hata hivyo, mradi wa umemejua kijijini hapo ni zao la ufadhili walioupata kutoka wafadhili; taasisi ya Energy and Environment Partnership (EEP) kiasi cha Euro 263,000 (Sh.mil 689); Taasisi ya Kuendeleza Mitaji ya Umoja Mataifa (UNCDF) Dola za Marekani 124,000 (Sh.mil 285) na Ensol inayogharamia asilimia 20 ya fedha za mradi ambazo ni Dola za Marekani 120,000 (Sh.mil 276).

**Wasimamizi wa serikali**

Bosi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura), ambako Victor Laabaa, akielezea mkakati wa kupunguza bei hizo kwamba: "Katika kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini wananufaika na nishati sawa na wale wa mijini, tunatengeneza kikokotoo ambacho kitapima na kudhibiti gharama za juu za nishati, ili kudhibiti bei zinazowekwa na wawekezaji wa umeme."

Hata hivyo, bado kuna mtazamo wa jumla kwamba uwapo wa nishati hizo vijijini, umesaidia kumpunguzia mwanamke muda mwingi wa kutafuta vyanzo mbadala vya nishati.

Mtaalamu wa Nishati kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Kamugisha Byabato, anasema wanawake ndio waratibu wakuu ndani ya familia, hivyo kuwapo umeme kwao kunawapunguzia muda mwingi wanaoutumia kutafuta mbadala wa nishati.

Dk. Bayabato anataja baadhi ya mifano ya mbadala huo majumbani, ni kutafuta kuni, kuchota maji na kutafuta mafuta ya taa.



Wabunge wakiwa katika mjadala juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Wabunge wamuweka May kitimoto hoja EU

**LONDON,** Uingereza

BUNGE nchini, limepinga mapendekezo yote manane yaliyotolewa mbadala kwa mpango wa Brexxit wa Waziri Mkuu Theresa May.

Bila ya mpango mpya Uingereza, italazimika kuondoka Umoja wa Ulaya bila ya mkataba ifikapo Aprili 12, mwakani.

Wabunge walipiga kura Jumatano usiku juu ya njia mbadala zitakazoweza kutumika kuutatua mkwamo katika mpango wa Brexit. Njia hizo mbadala ni pamoja na:

Kuondoka EU bila mkataba, Kubakia Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja la jumuia; kuitisha kura ya maoni juu ya mkataba wowote utakaofikiwa; kuubatilisha mchakato mzima wa Brexi, kama hakuna matarajio ya kufikia makubaliano.

Waziri Mkuu May, anakabiliwa na shinikizo linaloongezeka kutoka kwa wabunge wanaounga mkono mchakato wa Brexit katika chama chake cha Conservative, wanaomtaka aachie madaraka.

Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani, Boris Johnson, alishatangaza kuwa safari hii ataunga mkono mpango wa Waziri Mkuu, ambao awali aliupinga.

Inaelezwa kuna uwezekano mkubwa, Boris Johnson, ndiye atakayechukua mahala nafasi ya Theresa May, iwapo atajuzulu.

Pia, Chama cha Democratic Union (DUP) cha Ireland ya Kaskazini, kinachoiunga mkono serikali ya May kwa viti vingi bungeni, kimetangaza kuupinga mpango wa Waziri Mkuu huyo. Imedai ni mpango hatari kwa umoja kati ya Ireland na majimbo mengine ya Uingereza.

Inadaiwa, uamuzi huo unaihatarisha Uingereza kunasa kiuchumi katika EU.

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 183,958.3/- | ULEZI 144,052.6/-| MTAMA 80,857.14/-| VIAZIMVIRINGO 71041.67/- **FEDHA >>** RAND 157.06 | KSH 22.80 | USH 0.62 | RSH 2.55|

UCHUMI

# HUJAFA HUJAUMBIKA KWA FAUSTINA...

## Ulemavu ghafla ulimgeuza mjamzito tegemezi, sasa ahudumia kundi

- Alipelekwa ugenini, akaja na mbinu za uchumi
- Asimamia familia pekee; mkurugenzi wa taasisi

**Na Mary Mosha,** HAI

KUNA usemi: "Pale mwanadamu anapoishia ndipo Mungu anapoanzia."

Hili ndilo lililojitokeza kwa Faustina Urassa (38) baada ya madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Rufani KCMC kuthibitisha hana uwezo tena wa kutembea kwa miguu yake. Chanzo ni ajali ya gari aliyoipata, huku akibainika alikuwa na ujauzito wa siku tisa.

Faustina anasimulia mkasa kwamba, mwaka 2000 akiwa anajianda kwenda katika shughuli zake za ujasiriamali, alipata ajali ya gari iliyomsababishia kupata matatizo ya uti wa mgogo na kumpoteza uwezo wa kutembea.

"Nilikimbizwa katika Hospitali ya Rufani KCMC, huku ndugu zake, jamaa na marafiki wakinikimbilia kuokoa uhai wangu na mume niliyekuwa naye akijitahidi kutimiza majukumu yake kwa mkewe (mimi),"anasema Faustina.

Mama huyo anasema, baada ya kupatiwa matibabu kwa muda wa wiki mbili, simanzi kubwa ilitanda kwa marafiki zake, mumewe baada daktari mkuu kuwathibitisha kuwa, hana uwezo wa kutembea tena.

Faustina anasema, ndipo wingu nzito ilimtandia ghafla, pale marafiki waliokuwa wanamhangaikia walipotea ghafla na anadai mumewe, hali kadhalika alitoweka kwa takribani miezi mitatu.

Anasimulia mkasa huo, huku kilichotokea kwa ndugu zake waliangukia msemo 'Hakuna Kondoo aliyelemewa na mkia wake,' kwani waliendelea kumuguza na kunitia moyo kwa mengi.

"Sikuumia sana moyoni, kwa kuwa sikuwa natambua haki zangu kama mlemavu. Niliona kuwa mume wangu alikuwa na haki ya kufanya hivyo, kwani sikuwa na uwezo wa kutembea tena, pia sikujiona kama binadamu wa kawaida.

"Lakini, ndugu zangu walikaa nami kwa muda wa mwaka mmoja katika kuhakikisha wanapata ufumbuzi wa tatizo lililonikumba. Nilipata mateso mengi kutokana na hali yangu ya ujauzito.

"Sikuwa naweza kujisaidia chochote, kwani haja kubwa na ndogo nilikuwa sina uwezo wa kuvizuia...hali 'iliyopelekea' (iliyomfanya) kupewa uangalizi maalumu chini ya madakati bingwa kwa muda wa miezi tisa," anasimulia huku akilengwa na machozi.

Faustina, anayewaorodhesha aliyobaki nao katika mapambano hayo, wazazi na ndugu wengine, akikumbuka alfajiri Machi 19, 2001, ghafla uchungu wote wa kutengwa uliangukia katika furaha, baada ya baadhi ya ndugu, mume na wakwe kuisikia sauti ya mtabibu "hongera mama, umejaliwa mtoto wa kike,"

Anasema, kuanzia hatua hiyo, mawazo yote yalihamia kwa mwanawe anayemtunza pasipo kuwa tegemezi kwa familia yake.

> **"Lengo letu ni kuona mwanamke anajitambua, anajua haki zake na anajikwamua kiuchumi na kuacha tabia ya kuomba omba kwa kisa ni mlemavu,"**



Faustina Urassa (kulia), akiwa na mnufaika wa mradi wake Jenifa Mushi na mwanawe. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA.**



Faustina anajitambulisha kuwa ni mtoto wa tano, katika familia ya watoto saba, ya Mzee Jonathan Urassa.

**Ujasiriamali ulipoanza**

Mama huyo anakumbuka mwanzo safari yake ya kujikimu, ilianzia kufuma na kuuza vitambaa kwa watu mbalimbali waliomzunguka na walioleta na ndugu zao, akiuza dazeni ya vitambaa kwa Sh. 9,000.

"Wakati mwingine wateja walikuwa wakisumbua malipo, kwani sikuwa na uwezo wa kuwafuata walipo, lakini sikukata tama.

"Niliendelea kusonga mbele na wazazi walijitajidi katika kuninunulia 'kiti mwendo.' Biashara hiyo niliifanya kwa kipindi cha mwaka na nusu," anasema.

Anaendeleza simulizi kwamba, mara baada ya mwanawe kutimiza umri wa miezi nane, alikutana na asasi iitwayo Kilimanjaro Assosiaton of Spinal Cord Injured, (Chama cha Majeruhi wa Uti wa Mgongo), walimtaka aungane nao, wampeleke nchini Afrika ya Kusini mafunzo ya kujikimu.

Anasema ilimchukua muda mrefu kukubali, kwani alijawa na hofu ya namna ya kumuacha mwanawe, huku akiwa na changamoto kuhusu namna ya kujitegemea huduma ya kijisaidia, kuligana na uhalisia wa maisha yake akiwa huko ughaibuni.

"Baada ya mazungunzo na muda mrefu na ndugu zangu, na kupata uhakika wa mtu wa kukaa na mtoto wangu, niliamua kwenda, ingawa nilikuwa na hofu nani atakayeweza kunisaidia, wakati ninapokumbwa na haja,: anatamka.

"Kwa sababu, baada ya kupata ajali, sikuwa na uwezo wa kuzuia aja ndogo wala kubwa.....baada ya kupata ushauri wa kisaikologia nilienda," anafafanua.

**Mwanzo mpya Afrika Kusini**

Mjasiriamali Fausine anaeleza baada ya kufika nchini Afrika ya Kusini, alianza kujifunza kwa vitendo alipowaona walemavu wenzake wakijihudumia katika kila kitu, hali iliyomfanya ajiamini katika kuiga, huku wakipewa mafunzo juu ya haki zao na namna ya kujiendeleza kiuchumi.

Anasema, baada ya kuhitimu mafunzo alitunukiwa cheti kama mkufunzi wa mafunzo rika na alirejea nyumbani na kuanza kufanya kazi na shirika la Kasi, kwa muda wa miaka tisa, kisha akahamia shirika la Motivation Tanzania kwa miaka sita, hatua zilizompa fedha za kuhudumia familia yake.

"Niliweza kununua eneo na kujenga nyumba ya vyumba vinne, stoo, jiko, sehemu ya kufuga kuku na bata katika kijiji cha Msasani, kilomita 16 kutoka stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani. Nikaweza kuishi na mtoto wangu ambaye 2018 alihitimu kidato cha nne katika shule ya Fountain of Hope, na kupata ufaulu daraja la pili," anasimulia.

Anaeleza anavyojimudu kiuchumi, kwamba hivi sasa anahudumia familia ya watu sita, inayoundwa na wafanyakazi wawili, pia watoto wa kaka na dada zake.

Mama huyo anasema, yake kiu kwa sasa ni kuihudumia jamii ya watu waliopatwa na matatizo ya uti wa mgongo, kwani amegundua katika jamii watoto wa kike wanakabiliwa changamoto nyingi.

**Aanzisha shirika**

Fausina anasema, mwaka 2017 alianzisha shirika la Songambele Initative Organisation, inayohusika na kuwasaidia wanawake wenye ulemavu, yeye akiwa mkurugenzi na linafanya kazi mkoani Kilimanjaro,

Kwa sasa taasisi hiyo ina wanachama 150, ingawaje anasema katika upande wa pili walio hai ni 60 ( asilimia 40 ) tu huku wengine 70 ( asilimia 46.6) wanaokabiliwa na hali ngumu ya maisha, ikiwemo kukosa simu na kushindwa kuwasiliana kwa wakati.

"Lengo letu ni kuona mwanamke anajitambua, anajua haki zake na anajikwamua kiuchumi na kuacha tabia ya kuomba omba kwa kisa ni mlemavu," anasema

**Wafanyakazi wenzake?**

Abdul Munishi, ni Mratibu katika shirika la Songambele, akiwa ni mlemavu wa uti wa mgongo, anakiri changamoto nyingi zinakabili, pia wanakosa ushirikiano kutoka kwa mashirika mengine, hali inayowakwamisha kutimiza majukumu yao ya kuihudumia jamii kimaendeleo na mahitaji mengi binafsi.

"Mbali na kukosa fedha na mikopo katika halmashauri, tunakabiliwa na changamoto ya kukosekana ushirikiano kutoka mashirika ambayo yanafanya kazi nyingine, hali inayotufanya tushindwe kuwahudumia walemavu wote wanaofika katika ofsini yetu," anasema.

Faisine anasema, walemavu wengi wanakabiliwa na changamoto ya miundombinu katika halmashauri, mikoa na kumbi za mikutano, ambazo wanaweza kuzituma kufanyia mikutano mbalimbali na wanachama wao.

**Wanufaika**

Mlemavu Jenifa Masawe (33), ni mama wa watoto watatu, ambaye ajali yake aliipata alipoanguka akikata majani kijijini kwao Kibosho, Kilimanjaro. Ni ajali iliyomsababishia ulemavu katika uti wa mgongo na hadi sasa hawezi tembea tena.

"Mume wangu alinikimbia na kuninyang'anya watoto wawili. Nasikia wanaishi eneo la... na tayari ana mwanamke mwingine.

"Mama yangu anashida ya afya ya akili. Ndugu zangu alinifukuza baada ya kuona ni mlemavu. Nashukuru Mungu, shirika hili liliweza kunisaidia kupata kiti mwendo kilichonisaidia kushughulika katika maeneo mbalimbali, ikiwawo kumhudumia mwanangu," anasema.

"Sina nyumba ya kukaa, nimeazimwa chumba kimoja, kutokana na uchanga wa shirika hili na uhitaji bado ni mkubwa, kwa kuwa walemavu wengi wana matatizo kama yangu.

"Tunaiomba serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali, hata watu binafsi kutusaidia angalau kupata mtaji utakaotuwezesha kujikimu kimaisha na kuondoa utegemezi," anasema

# BIASHARA KATIKA PICHA



Rais mstaafu, Benjamin Mkapa (kulia), akipeana mikono na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alipomtembelea ofisini kwake, akiwa na Meneja Uhusiano wa benki hiyo, William Kallaghe (kushoto), Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**



Mfanyabiashara wa matunda akimuuzia mteja wake katika soko la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: HALIMA KAMBI**



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (katikati), pamoja na viongozi wengine wakifurahia wakati wa hafla ya kuzindua Tawi jipya la Benki ya Biashara Mkombozi mkoani Iringa jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela. **MPIGAPICHA WETU**

BEI YA MAZAO >>MAHINDI 52,620/- | MAHARAGE 176,041.7/-| NGANO 1130,066.7

UCHUMI

# Wajipanga kukagua uchumi wa miaka 25 kutoka safari Beijing

**Na Yasmine Protace**

WADAU wa maendeleo kutoka asasi za kiraia na TGNP - Mtandao na Haki Elimu, walikutana jijini Dar Es Salaam, kufanya mapitio ya hiari ya kitaifa kuhusu utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Dunia, wakitaja mahsusi lengo namba nne na tano, pamoja na viashiria vyake.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP - Mtandao, Lilian Liundi, anasema warsha imelenga kuainisha na kutambua wadau waliojikita katika utekelezaji wa lengo wa malengo hayo.

Lilian anasema, kunatarjiwa kufanyika tathmini kuanzia ngazi ya jamii na taifa, akifafanua: "Tathimin hiyo itajadili maeneo ya kujengeana uwezo katika malengo tajwa na kuwekwa mikakati na makubaliano ya pamoja juu ya ufuatiliaji tathimini na utoaji taarifa ya utekelezaji wa maeneo tajwa."

Anaongeza kuwa, TGNP - Mtandao na Haki Elimu, ni miongoni mwa wanachama wa Jukwaa la Malengo ya Maendeleo Endelevu Tanzania na wamejitolea kuratibu mchakato wa mashauriano, kuhusu utekelezaji wa malengo hayo Namba Nne na Tano.

Anasema, hiyo ni sehemu ya maandalizi ya taarifa ya mapitio ya hiari kitaifa, kuhusu utekelezaji wa malengo ya Maendeleo Endelevu, inayotarajiwa kuitumia, Julai mwaka huu.

Lilian anakumbusha kwamba Maendeleo Endelevu, yaliridhiwa wakati serikali upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, ) zilipoandaa mpango wa Maendeleo wa Kitaifa ya Miaka Mitano Awamu ya Pili ( FYDP 11) na Mkakati wa Kupunguza na Kutokomeza Umasikini Zanzibar ( MKZA111).

Anasema, ni mpango ulioingiza malengo ya maendeleo endelevu katika vipaumbele vya yalivyoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa na Ajenda ya Umoja wa Afrika mwaka 2063.

Liundi anasema nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, ziliamua haja ya kufanya mapitio ya hiari kitaifa, kila mara wanapokutana katika majukwaa yao ya kisiasa .

Anasema ni mapitio yatakayowakilishwa na nchi zilizoendelea, zinazoendelea, taasisi za Umoja wa Mataifa na wadau mbalimbali, asasi za kiraia na sekta binafsi..

Amasema, serikali imeamua kushiriki katika mchakato huo wa mapitio ya hiari ya kitaifa, mchakato ambao unahitimishwa na mkutano mkubwa wa Umoja wa Mataifa, unaotarajiwa kufanyika mwezi Julai kila mwaka.

"Kwa mara ya kwanza, nchi yetu itawasilisha taarifa yake ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, mnamo mwezi Julai mwaka huu. Hata hivyo, tunatarajia nchi yetu itaendelea kushiriki katika mchakato huu kila mwaka hadi ifikapo 2030," anasema.



Kinamama wajasiriamali wakiwa kazini, kutekeleza ajenda ya mkutano wa Beijing, China.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Katika kipindi hicho cha miaka 25 ya Beijing tutaona hali ikoje na mabadiliko yaliyopatikana, yatajulikana kutokana na kutimia miaka 25,"**



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP - Mtandao, Lilian Liundi

Mkuu wa Idara ya Ujenzi wa Nguvu za Pamoja kutoka TGNP Mtandao, Grace Kisetu, anasema mpango wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, wanagusa lengo linalomwanangalia mwanamke kuwezeshwa kiuchumi, ikiwamo usawa katika uongozi.

Anaeleza imani yake kwamba, itasaidia kufikiwa malengo hayo na TGNP Mtandao imekuwa ikisaidia harakati mbalimbali zinazowawezesha kinamama kujitambua na wanazijua haki zao za usawa katika uongozi na mgawanyo wa majukumu.

Lilian anaahidi ifikapo mwakani, itakuwa miaka 25 ya Siku ya Wanawake Duniani kwa Watanzania walioenda Beijing kutoka hapa nchini.

"Katika kipindi hicho cha miaka 25 ya Beijing tutaona hali ikoje na mabadiliko yaliyopatikana, yatajulikana kutokana na kutimia miaka 25," anasema.

**KUTOKA KWA WADAU**

Martina Rumanyila, Mkurugenzi wa asasi ya Heardh, iliyopo Arusha anajitambulisha kuwa wanachama wa TGNP - Mtandao na asasi yake

inaendeleza masuala ya kijinsia na malengo endelevu ya maendeleo, wakisimamia la tano.

Anasema, mwaka 2030 wanatarajia watatahmini walichokifanya, kutokana na kuendelezwa usawa wa kijinsia na katika kufanya kazi zao, wanakumbana na changamoto kama ndoa za utotoni na kuwafanya kushindwa kufikia malengo hayo.

Kwa mujibu wa Martina, wanakabiliana na changamoto katika baadhi ya shule, kutokuwa na maji, vyoo, hata kusababisha wasichana kushindwa kuhudhuria masomo na wengine wanaacha.

"Watoto wa kike wanapokuwa katika siku zao shule kama haina maji watoto hao hawawezi kuhudhuria masomo," anasema.

Anaongeza kuwa, sheria ya ndoa za utotoni ina changamoto kubwa na imekuwa ikichangia hata lengo namba tano kutolifikia vizuri.

Raymond Maenda, anatoka katika asasi ya Umoja wa Mataifa (UN) ambao pia ni waratibu wa Jukwaa la Maendeleo Endelevu, anasema suala la elimu limekuwa changamoto kubwa katika kutimiza lengo husika.

Maenda anasema, kuwapo elimu ya bure, kumewaenda vizuri wanafunzi kuandikishwa darasa la kwanza kwa idadi kuwa, pia wanaomaliza elimu msingi wanafuatiliwa iwapo ameingia kidato cha kwanza.

Anafafanua kuwa wanaomaliza elimu ya kidato cha nne wanafuatiliwa idadi ya wanaoendelea kidato cha tano, ingawa katika sura ya pili kuwapo changamoto za mimba za ututoni, wanafunzi wanaacha shule kutokana na mimba.

Mwakilishi huyo wa Umoja wa Mataifa, anashauri kuboreshwa miundombinu inayoonyesha kuwa na changamoto, ikiwamo kuwawekea vyoo shule, kama nyenzo za kuwasaidia umaliza shule vyema.

Mwemezi Makumba, Meneja wa Utafiti, Ubunifu na Uchambuzi na Sera wa HakiElimu, anasema wanaangalia malengo ya Maendeleo Endelevu namba nne, linaloangalia upatikanaji kielimu ifikapo mwaka 2025.

Anaongeza kuwa, malengo ya 2030 yanataka kila mtoto awe shule ajifunze elimu itakayomsaidia na anafafanua kuwa Tanzania ya Viwanda, ni sehemu ya uchumi wa viwanda kitaifa na kimataifa. Makumba anakiri katika sekta ya elimu, serikali imepiga hatua na ombi lao kwa serikali ipokee maono ya wadau na kuyafanyia kazi stahiki.

/- |UWELE 84,000/- **FEDHA >>** USD 2,300.90 | PAUNI 3,043.40 | EURO 2,593.80 |

BIASHARA




Mkutano wa biashara Afrika, mwaka jana jijini Kigali, Rwanda. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Kagame ang'aka namna Afrika inavyojimaliza kupitia biashara

## • Mzigo wa Mombasa 'dezo' kufika China, kuliko Kigali

**KIGALI,** Rwanda

KONGAMANO la kuchambua fursa za kibiashara barani Afrika, litafanyika jijini Kigali Rwanda na kuhudhuriwa na wakurugenzi wa kampuni mbalimbali kubwa, pia marais barani Afrika.

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, anasema mikakati yote ya kimaendeleo inayochukuliwa barani Afrika kwa kiasi imeshindwa kufikia lengo kutokana na sababu za kisiasa.

Rais Kagame, alikuwa akizungumza jijini Kigali mwanzoni mwa kikao cha siku mbili kinachowajumuisha wadau wa maendeleo zaidi ya 1,500 pamoja na viongozi wa baadhi ya serikali za mataifa ya Afrika.

Ni Kongamano ambalo mbali na wakuu wengi wa kampuni kubwa za kiuchumi na biashara barani Afrika, linahudhuriwa na marais Faure Gnasingbe wa Togo, Felix Tshishekedi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Sahle Work Zewde wa Ethiopia.

Ni kongamano ambalo kwa kiasi kikubwa, linachambua fursa za kibiashara barani Afrika, changamoto zake na nini sekta binafsi pamoja na serikali za Kiafrika zinapaswa kufanya, ili kuondoa adha hiyo inayoodhofisha ushirikiano wa kibiashara baina ya Waafrika.

Phillipe Le Houerou, ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa kuhusu fedha (IFC), anayesema Afrika inahitaji kutekeleza mikakati kutokana na mahitaji yaliyopo.

"Afrika inahitaji fursa mpya za ajira zinazofikia milioni moja na laki saba kila mwezi. Ni kwa jinsi gani unatengeneza fursa hizo?

"Ni kutengeneza sekta binafsi yenye nguvu na yenye ushawishi mkubwa na inayowezeshwa na mazingira huru ya kufanya biashara katika bara zima."

Gharama za usafirishaji anazitaja nazo kuwa tatizo, hasa miongoni mwa Waafrika, kama anavyobainisha Profesa Carlos Lopes, kutoka Chuo Kikuu cha Cape Town, Afrika Kusini.

> **"Vilevile kuna mamilioni ya lita za maziwa yaliyokuwa yakisafirishwa kutoka Rwanda kuelekea nchini Kenya kwenye viwanda vya Kenya hayo yalizuiliwa pia kwa miezi hadi yakaharibika"**



Rais Paul Kagame, akizungumza kwenye kongamano hilo

Profesa Lopes, anatoa mfano linganishi kuwa, gharama za usafirishaji kontena kutoka Rwanda hadi Mombasa, ni kubwa kuliko kutoka Mombasa hadi China.

Inaelezwa ni hali isiyokubalika na suluhisho hilo ni kuwa na Soko la Pamoja la Afrika (CFTA) kufikia maboresho kama hayo, kunahitaji mazungumzo yenye tija.

Pia, anataja mazingira huru yanayotajwa, ni sawa na hayapo miongoni mwa mataifa ya Kiafrika, kutokana na ukweli kwamba ni kinyume na kilichoko majukwaani.

Rais Paul Kagame, katika ufafanuzi wake, anataja kuwapo tatizo la kuingiza siasa nyingi katika majukumu, akitoa mfano wa sura ya msuguano kati ya Rwanda na Uganda.

"Tuna mamia ya watu kutoka Rwanda wanaokamatwa na kuzuiliwa kwenye sehemu zisizofahamika kule Uganda. Hii inapoendelea ni sawa na kuwaambia watu kwamba hawatakiwi kule Uganda.

'Hili ni suala ambalo mimi binafsi nimelizungumzia na utawala wa juu kule Uganda kwa muda wa miaka miwili sasa, lakini halipatiwi ufumbuzi," anasema Rais Kagame.

"Lakini hilo tuliweke kando kidogo kuhusu athari za uchumi. Kuna makontena yetu na madini yaliyozuiliwa nchini Uganda wakati yakielekea Mombasa nchini Kenya kwa muda wa miezi mitano. Haya si makontena ya raia wa Rwanda, hapana yalikuwa ni mwekezaji wetu kutoka Ujerumani.

"Vilevile kuna mamilioni ya lita za maziwa yaliyokuwa yakisafirishwa kutoka Rwanda kuelekea nchini Kenya kwenye viwanda vya Kenya hayo yalizuiliwa pia kwa miezi hadi yakaharibika", anasema Rais huyo.

Na hii pengine ikawa sababu japo bila kutajwa, ikaifanya Rwanda kuweka nguvu za ushirikiano wa kibiashara na mataifa ya mbali kama vile Gabon na mengine ya kati na Magharibi mwa Afrika.

Wiki iliyopita Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zilitia saini makubaliano ya ushirikiano wa safari za anga kwa ndege ya Rwanda, Rwandair itaanza safari za moja kwa moja baina ya Kigali na Kinshasa kuanzia, April 15.

**DW**

# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Machi 27, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Manyara | Mbeya | Morogoro | Mtwara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 46,000 | 70,000 | 53,000 | 60,000 | 40,000 | 45,000 | 51,000 | 42,000 | 48,000 | 48,000 |
| Mchele | 200,000 | 210,000 | 195,000 | 185,000 | 180,000 | 160,000 | 200,000 | 175,000 | 165,000 | 190,000 |
| Mtama | 38,000 | 60,000 | 35,000 | 100,000 | 80,000 | 100,000 | 42,000 | 105,000 | 71,000 | 100,000 |
| Uwele | 40,000 | 60,000 | 34,000 | 110,000 | NA | 100,000 | 100,000 | NA | 71,000 | NA |
| Ulezi | 72,000 | 140,000 | 75,000 | 150,000 | 180,000 | 150,000 | 120,000 | 120,000 | 155,000 | 190,000 |
| Ngano | 90,000 | 130,000 | 160,000 | NA | 98,000 | 150,000 | 120,000 | 130,000 | 163,000 | NA |
| Maharage | 155,000 | 220,000 | 170,000 | 150,000 | 180,000 | 140,000 | 150,000 | 210,000 | 185,000 | 180,000 |
| Viazi Mviringo | 70,000 | 80,000 | 66,000 | 75,000 | 50,000 | 90,000 | 50,000 | 50,000 | 82,000 | 115,000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Machi 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam

Kikao cha Machi 27, 2019

**Muhtasari**

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,477.39 | -4.11 |
| DSEI | 2,066.89 | -2.11 |
| Thamani za Hisa (bln) | 19,922.46 | |
| Mauzo | 163,344,640.00 | |
| Hisa | 1,024,036 | |

**Zilizopanda na Zilizoshuka**

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| SWIS | 1,700 | -15.00% |
| EABL | 4,660 | -0.43% |
| KA | 115 | -4.17% |
| USL | 15 | +50.00% |
| ACA | 6,150 | +0.82% |

**Viwango vya kubadilisha**

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Machi 27, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 6,150 | 6,100 | +0.82 |
| CRDB | 125 | 125 | +0.00 |
| DCB | 340 | 340 | +0.00 |
| DSE | 1,300 | 1,300 | +0.00 |
| EABL | 4,660 | 4,680 | -0.43 |
| JHL | 9,600 | 9,500 | +1.05 |
| KA | 115 | 120 | -4.17 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,000 | 1,000 | +0.00 |
| MBP | 490 | 490 | +0.00 |
| MCB | 500 | 500 | +0.00 |
| MKCB | 800 | 800 | +0.00 |
| MUCOB | 400 | 400 | +0.00 |
| NICO | 165 | 165 | +0.00 |
| NMB | 2,340 | 2,340 | +0.00 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TBL | 11,400 | 11,400 | +0.00 |
| TCC | 17,000 | 17,000 | +0.00 |
| TCCL | 600 | 600 | +0.00 |
| TICL | 385 | 385 | +0.00 |
| TOL | 660 | 660 | +0.00 |
| TPCC | 2,020 | 2,020 | +0.00 |
| TTP | 120 | 120 | +0.00 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 22.62 | 22.80 |
| UGANDA SHS | 0.58 | 0.62 |
| RWANDAN FRANC | 2.52 | 2.55 |
| BURUNDI FRANC | 2.18 | 2.20 |
| USD | 2278.12 | 2300.90 |
| POUND STG | 3012.58 | 3043.40 |
| EURO | 2566.98 | 2593.80 |
| CANADIAN $ | 1698.06 | 1714.53 |
| SWITZ. FRANC | 2291.18 | 2313.16 |
| JAPANESE YEN | 20.62 | 20.82 |
| SWEDISH KRONOR | 246.02 | 248.40 |
| NORWEG. KRONOR | 264.86 | 267.42 |
| DANISH KRONOR | 343.88 | 347.26 |
| AUSTRALIAN $ | 1613.59 | 1630.88 |
| INDIAN RPS | 33.07 | 33.39 |
| PAKISTAN RPS | 15.44 | 16.32 |
| ZAMBIAN KWACHA | 185.62 | 188.60 |
| MALAWIAN KWACHA | 2.91 | 3.10 |
| MOZAMBIQUE-MET | 35.93 | 36.23 |
| ZIMBABWE $ | 0.43 | 0.43 |
| SDR | 3173.12 | 3204.85 |
| GOLD (T/O) | 2994609.96 | 3026327.75 |
| S. AFRICAN RAND | 155.62 | 157.06 |
| UAE DIRHAM | 620.27 | 626.35 |
| SINGAPORE $ | 1682.26 | 1698.08 |
| HONK KONG $ | 290.25 | 293.14 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 607.45 | 613.51 |
| KUWAIT DINAR | 7502.20 | 7574.98 |
| BOTSWANA PULA | 210.95 | 213.52 |
| CHINESE YUAN | 338.85 | 342.18 |
| MALAYSIA RINGGIT | 559.73 | 564.64 |
| SOUTH KOREA WON | 2.00 | 2.02 |
| NEWZEALAND | 1547.07 | 1563.46 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **27/Mar/2019** | **3.10** | **2,313.75** | **2,298.50** | **2,300.90** |
| 26/Mar/2019 | 3.00 | 2,313.00 | 2,298.55 | 2,300.92 |
| 25/Mar/2019 | 2.50 | 2,310.00 | 2,298.60 | 2,300.89 |
| 22/Mar/2019 | 3.20 | 2,315.00 | 2,298.65 | 2,300.91 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **27/Mar/2019** | **57,000** | **5.50** | **5.00** | **5.07** |
| 26/Mar/2019 | 35,000 | 6.00 | 5.00 | 5.21 |
| 22/Mar/2019 | 30,000 | 5.30 | 5.00 | 5.10 |
| 21/Mar/2019 | 66,450 | 6.50 | 5.00 | 5.37 |
| 20/Mar/2019 | 66,450 | 6.50 | 5.00 | 5.68 |
| 19/Mar/2019 | 15,650 | 6.50 | 4.00 | 5.70 |

# Rais China awapa mwelekeo mabosi uchumi wa dunia



RAIS Xi Jinping (pichani)wa China, amehimiza nchi mbalimbali duniani kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto zinazozikabili, badala ya kubaki kimya.

Akihutubia hafla ya kufungwa Kongamano la Usimamizi wa Dunia kati ya China na Ufaransa juzi, amesisitiza kwamba kutokana na changamoto kubwa za kimataifa, nchi mbalimbali zinapaswa kuchukua hatua.

Hafla hiyo iliwashirikisha Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa, Chansela wa Ujerumani, Angela Merkel na Mwenyekiti wa Kamati ya Umoja wa Ulaya Jean Juncker.

China na Ufaransa, zikiwa washiriki muhimu wa usimamizi wa dunia, zina maoni mengi ya pamoja yakiwemo kudumisha amani, usalama na utulivu duniani, kulinda utaratibu wa pande nyingi wa biashara huria na kuunga mkono Umoja wa Mataifa kufanya kazi chanya.

"China na Ufaransa zinafuata kanuni ya kimsingi ya uhusiano wa kimataifa ikiwa ni pamoja na kuheshimiana na kuaminiana, kutendeana kwa usawa, kufungua mlango, kusikilizana, kunufaishana ili kupata mafanikio kwa pamoja."

Anafafanua Rais Jinping, kwamba: "Kukamilisha usimamizi wa dunia na kuwa nguvu muhimu ya kulinda amani na utulivu duniani na kuhimiza maendeleo ya ustaarabu wa binadamu."

Hivi sasa dunia inakabiliwa na mabadiliko makubwa na Rais Xi Jinping ametaja mpango wa nchi yake kukabiliana na changamoto tajwa, akisisitiza pia nchi zingine duniani zinapaswa kubeba majukumu kimataifa na kuchukua hatua halisi. Anazitaja:

"Kwanza, tunapaswa kushikilia haki katika utatuzi wa suala la usimamizi wa dunia. Pili, tunapaswa kushikilia kujadiliana na kuelewana katika utatuzi wa suala la uaminifu.

"Tatu, tunapaswa kushikilia ushirikiano katika utatuzi wa suala la amani. Na nne tunapaswa kushikilia kunufaishana katika utatuzi wa suala la maendeleo, "anasema.

Hivi sasa ni miaka 55, tangu China na Ufaransa zianzishe uhusiano wa kibalozi. Rais huyo anasema, nchi hizo mbili zinatakiwa kuelekeza dira mbali na kuongeza ushirikiano katika sekta mbalimbali.

**Rais Macron**

Rais Macron, naye anasema nchi yake inatilia maanani kazi nzuri ya China kimataifa, hivyo Ulaya na China zinapaswa kuongeza uaminifu.

"Pendekezo la 'Ukanda Mmoja, Njia Moja' lililotolewa na Rais Xi lina maana muhimu na linatoa mchango mkubwa katika kuhimiza utulivu wa dunia na kuwafanya watu wa nchi tofauti waishi pamoja kwa amani. Nchi za Ulaya zinaweza kujiunga na pendekezo hilo kwa njia ya kivumbuzi."

**Bibi Merkel**

Kiongozi wa Ujerumani, Bibi Merkel, anasema EU inapaswa kuharakisha mazungumzo ya makubaliano ya uwekezaji kati yake na China na kujadili ushiriki wake kwenye pendekezo la 'Ukanda Mmoja, Njia Moja.'

Anaitaka EU na China zishirikiane, kulinda utaratibu wa nchi nyingi na kujadili mageuzi ya mashirika ya kimataifa, likiwamo Shirika la Biashara la Kimataifa.

**Kutoka EU**

Aidha, kiongozi wa EU, Juncker, anasema , Umoja wa Ulaya na China ni wenza muhimu wa ushirikiano wa kimkakati, na muhimu kwa pande hizo mbili kudumisha mazungumzo sawa.

Kabla ya hafla hiyo, viongozi hao walifanya mazungumzo kuhusu uhusiano wa kimkakati kati ya China na EU kufikia maoni ya pamoja katika baadhi ya maeneo ya muafaka.

**Kwa mujibu wa China Radio International- CRI**



HABARI MBEYA

# Jinamizi la udumavu kwa watoto lapiga kambi Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa Mkoa wa Mbeya bado unakabiliwa na changamoto ya udumavu wa watoto licha ya kuwa miongoni mwa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Lishe kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Cecilia Mtega, wakati wa mafunzo maalumu ya uongezaji wa virutubisho kwenye vyakula yaliyoandaliwa na Mradi wa Nafaka unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Wananchi wa Marekani (USAID).

Mafunzo hayo yaliwahusisha waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari wa mikoa ya Mbeya na Songwe, wasindikaji wa nafaka hasa unga wa mahindi, wataalamu wa lishe kutoka katika Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa pamoja na baadhi ya wafanyabiashara.

Mtega alisema utafiti uliofanyika mwaka 2015 ulionyesha kuwa asilimia 37.7 ya watoto wanakabiliwa na udumavu, uzito mdogo asilimia 12.2, ukondefu asilimia 4.7 na upungufu wa damu asilimia 55 na kwamba hali hiyo inatokana na lishe duni.

Alisema kulingana na utafiti wake binafsi ambao sio rasmi ni kwamba asilimia kubwa ya watoto wanaokabiliwa na udumavu na wanatoka kwenye familia ambazo zimetelekezwa na mzazi mmoja hasa wa kiume na hivyo kupelekea wanawake kushindwa kumudu kuhudumia watoto.

Alisema baadhi ya wanawake wanaowapeleka watoto wao kwenda kutibiwa kutokana na matatizo ya lishe duni huwa wanakuwa hawana uwezo wa kumudu kuwapatia watoto wao lishe bora. "Tunashauri wazazi wote wawili washiriki katika kulea familia, kila mwanamke ambaye mtoto wake anakabiliwa na lishe duni, ukimuuliza baba wa mtoto yuko wapi unakuta wanasema alikimbia familia, sasa tunashauri wote washiriki," alisema Mtega.

Alisema baadhi ya familia zinazalisha chakula na kuuza chote bila kuacha ziada kwa ajili ya familia zao na hivyo akawataka wananchi kubadilika.

Kwa upande wake mtaalamu wa shughuli za Kilimobiashara na usindikaji kutoka kwenye Mradi wa Nafaka, Absalum Mwaipaja, alisema kwa sasa wanaendelea na mradi wa kuongeza virutubisho kwenye vyakula ili kukabiliana na changamoto za lishe nchini. Alisema mradi huo unafanya kazi na wasindikaji wa unga wa mahindi na vikundi vya wakulima ili kuungana na serikali katika kupambana na changamoto ya lishe duni. Aliongeza kuwa mradi huo unawaunganisha wazalishaji wa unga na wazalishaji wa mashine za kuchanganyia virutubisho hivyo pamoja na wazalishaji wa mifuko ili kuwasaidia wapate vifungashio hivyo kirahisi.

"Wananchi wengi wamekuwa wakitumia vyakula ambavyo havina virutubishi, hivyo serikali iliamua kuanzisha taratibu za kuweka virutubisho hivyo kwenye unga na chumvi ili wavipate huko," alisema Mwaipaja.

Hata hivyo alisema wataendelea na mradi huo kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaondokana na changamoto ya udumavu wa watoto kwenye mikoa ambayo ipo kwenye mradi.



Vijana walioji-ajiri kwa kubuni jiko linalotembea la kuchoma mishikaki na vitu mbalimbali wakiwa katika mawindo ya wateja Barabara ya Morogoro eneo la Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Jeshi la Polisi latangaza vita na Bajaj

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya madereva wa magari ya abiria maarufu kwa jina la daladala jijini Mbeya kugoma kufanya kazi na kusababisha usumbufu kwa wananchi, Jeshi la Polisi mkoani humo limewatangazia kiama madereva Bajaj.

Madereva hao waligoma kwa lengo la kuishinikiza serikali kuziondoa bajaji kwenye barabara kuu kwa madai kuwa zinafanya kazi ambayo inapaswa kufanywa na daladala na hivyo kusababisha kazi yao kuwa ngumu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema mgogoro huo ulimalizwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

Alisema katika kikao cha kamati hiyo kilichohusisha pande zilizokuwa zinasigana pamoja na mamlaka za serikali ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra), Chama cha Kutetea Abiria (Chakua) na kukubaliana bajaji zisipite barabara kuu.

Alisema kufuatia makubaliano hayo, Jeshi la Polisi litawakamata na kuwachukulia hatua kali madereva bajaji watakaokiuka makubaliano hayo kwa kuendelea kusafirisha abiria kwenye barabara kuu na kuchukua abiria kwenye vituo vya daladala.

Aliwataka kuendelea kutumia barabara na vituo ambazo wameainishiwa na kwamba jeshi hilo litaendelea kufanya doria na kuwakamata wote wanaokiuka makubaliano hayo.

"Kwenye kikao cha makubaliano na wao walikuwamo sasa hatutaki lililotokea hivi karibuni litokee tena, tunawakamata wote wanaokiuka makubaliano hayo na kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria," alisema Matei.

Aidha, aliwataka madereva wote mkoani humo kuendelea kuheshimu sheria za usalama barabarani ili kuufanya mkoa huo kutokomeza kabisa ajali za barabarani ambazo katika siku za karibuni ziligharimu maisha ya watu wengi.

Alisema kwa sasa katika mkoa huo ajali za barabarani zimepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na jeshi hilo kuchukua hatua mbalimbali za kuzuia ajali ikiwamo kuweka utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita kwa awamu kwenye maeneo ya milima.

Alisisitiza kuwa lengo la Jeshi la Polisi ni kuhakikisha ajali za barabarani zinafikia sifuri na kwamba hilo linawezekana endapo kila mtumia barabara atazingatia sheria.

Hata hivyo baadhi ya madereva na makondakta wa daladala wanadai kuwa endapo majaji zitaendelea kuonekana kwenye barabara kuu, watagoma tena na kuziachia bajaji ndizo zifanye kazi ya kubeba abiria.

Ndani ya mwezi mmoja Jiji la Mbeya limekumbwa na mgomo wa daladala mara mbili na kusababisha wananchi kushindwa kufanya kazi zao kwa amani kutokana na gharama za usafiri kuwa juu, ambapo bajaji zilikuwa zinawasafirisha kwa shilingi 1,000 kwenye maeneo ambayo daladala huwa zinawasafirisha kwa shilingi 400.

# Mamlaka ya maji yatahadharisha 'vishoka'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mbeya (Mbeya- WSSA) imewatahadharisha mafundi wa mitaani maarufu kwa jina la 'vishoka' wanaowaunganishia wananchi maji kuwa watachukuliwa hatua za kisheria.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja kutoka Mamlaka hiyo, Neema Stantoni, wakati alipokuwa anazungumza na gazeti hili kuhusu utendaji kazi wa mamlaka hiyo.

Neema alisema kuwa kuna baadhi ya watu ambao wamekuwa wakitumia mwamvuli wa mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira kuwaunganishia maji wananchi wakati sio watumishi wa mamlaka hiyo.


Alisema watu hao wamekuwa wakiisababishia serikali hasara kwa kuwa watu wanaounganishiwa maji wanakuwa hawapo kwenye mfumo rasmi, hivyo serikali inashindwa kuwatoza ankra ya maji wanayoyatumia wateja hao.

Neema alisema watu hao pia wamekuwa wakitumika mitaani kutengeneza miundombinu ya maji iliyoharibika bila mamlaka kuwa na taarifa wakati ndio yenye jukumu la kutengeneza na kuhakikisha miundombinu hiyo inakuwa na hali nzuri wakati wote.

"Mwananchi anapohitaji kuunganishiwa maji au anapoona mtandao wa maji umeharibika anapaswa kufika ofisini kwetu kutoa taarifa au kutupia simu ili mafundi wa mamlaka wafike kwa ajili ya kuwasaidia wateja wetu," alisema Neema.

Katika hatua nyingine Neema aliwataka watumiaji wa huduma ya maji kulipa ankra kwa wakati ili mamlaka hiyo iweze kujiendesha na kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi kwa wateja wake.

Alisema Mbeya-WSSA, inategemea ankra ya maji kwa ajili ya kijiendesha ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu, kusambaza mtandao wa maji, kutibu maji pamoja na mishahara ya watumishi na uendeshaji wa ofisi, hivyo kutolipa ankra ni kuikwamisha mamlaka hiyo.





# Waziri Biteko aagiza mkakati kusaidia wachimbaji madini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameiagiza Bodi mpya ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini nchini(GST) kushirikiana na wataalamu kufanya utafiti wa madini maeneo mbalimbali ili kusaidia wachimbaji kuyatambua.

Aidha, aliitaka taasisi hiyo kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo ili waondokane na imani za kishirikina wakati wa uchimbaji madini.

Biteko alitoa kauli hiyo juzi, wakati akizindua bodi mpya ya taasisi hiyo, jijini hapo.

Alisema endapo maeneo yenye madini yatatambuliwa yatavutia wawekezaji katika sekta ya madini.

Akizungumzia kuhusu imani za kishirikina, Biteko alisema wachimbaji wengi huamini imani hizo kabla ya kuingia mgodini jambo ambalo si sahihi.

"GST mna kazi kubwa ya kutoa elimu ya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo ili waondokane na hii dhana potofu ambayo inawafanya waamini kuwa kutopata madini kunatokana na mazingira ya kishirikina, kuna mahali niliienda lakini siwezi kupataja watu kabla ya kuingia machimboni utengeneza duara na kumtanguliza mwanamke akiwa mtupu," alisema Biteko.

Alieleza kwamba GST inapaswa kutoa elimu kwa wachimbaji hao ili wachimbe kitaalamu zaidi badala ya kuamini njia za kishirikina, jambo ambalo litawacheleweshea kazi zao.

Aliongeza kuwa lengo ni kuona watu wanakuwa na elimu hiyo badala ya kutegemea imani za kishirikina.

Pamoja na hayo, aliwataka kutathmini utendaji wa kazi wao na kwamba serikali ilifanya marekebisho ya sheria ya madini mwaka 2010 ili iweze kuimarisha usimamizi katika sekta ya madini. Naye Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Justian Ikingura, alisema wana kila sababu ya kutekeleza maagizo hayo kwa kuwa ni muhimu kwa sekta hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bahi, Dk. Fatuma Mnganga, akisikiliza maelezo ya jinsi ya kumpasua panya kutoka kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Msalato katika mahafali ya kidato cha sita katika shule hiyo, iliyoko jijini Dodoma jana.
**PICHA: MPIGAPICHA**

# Wanafunzi wa kike kidato cha tano kusoma bure

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Mariam Ditopile, ametangaza neema ya kuwalipia ada wanafunzi wa kike wote watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule za serikali mkoani Dodoma.

Ditopile alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo.

Alisema ameguswa na jitihada zinazofanywa na Rais Dk. John Magufuli katika sekta ya elimu, hivyo ameamua kuwalipia ada wanafunzi hao.

"Natarajia kuzindua programu maalum ya kuwawezesha wasichana ambao wamefaulu kidato cha nne kwenda cha tano ambao watachaguliwa kujiunga kidato cha tano tuweze kuwafadhili ili waweze kupata elimu, hili jambo litaratibiwa na Ofisi ya Vijana Mkoa wa Dodoma pamoja kwa kushirikiana na Ofisi ya Elimu ya Mkoa kupitia maofisa elimu wa wilaya tutawatambua wangapi wamefaulu na wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano," alisema.

Alieleza kuwa katika ilani ya uchaguzi ya CCM sura ya nne kipengele cha 52 kinaongelea suala la elimu ambacho ni kiungo muhimu katika maendeleo ya wananchi na ameshuhudia hatua kubwa kwenye sekta hiyo kupitia elimu msingi bila malipo. Naye, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM( UVC-CM) Mkoa wa Dodoma, Billy Chidabwa, alisema umoja huo unatarajia kufanya ziara Aprili 29, mwaka huu ya kukagua miradi ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa ya kati (SGR), kituo cha mabasi ya Dodoma pamoja na soko la kisasa.

Alisema pia ziara hiyo itaangalia fedha za vijana ambazo zipo kisheria.

"Safari hii tutaenda kukutana na wale vijana ambao inasemekana wamenufaika kwa sababu ule utaratibu upo kwa mujibu wa sheria, kama tunasifika ni sehemu kubwa ya kukusanya mapato katika mkoa huu ni imani yetu tutasifika katika kupata mikopo kwa sababu ipo kwa mujibu wa sheria kwa sababu tumesikia vijana wenzetu wakisema wengine wanapata, wengine hawapati," alisema mwenyekiti huyo.

# Walimu, wanafunzi Chonama wasaidiwa baiskeli

**Na Mwandishi wetu,** BAHI

SHIRIKA lisilokuwa la liserikali la Secope kwa kushirikiana na watu wa Ujerumani wametoa baiskeli 140 zenye thamani ya Sh. milioni 58 kwa wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Chonama Wilaya ya Bahi ili kukabiliana na tatizo la umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni.

Wanafunzi wa shule hiyo wanakabiliwa na changamoto ya mazingira magumu na hivyo kuwalazimu kutembea zaidi ya kilomita 22 kwa siku kwa ajili ya kufuata masomo.

Kufuatia hali hiyo, shirika hilo lilitoa baiskeli hizo ili kuwarahisishia wanafunzi kuwahi masomo.

Akizungumza wakati akikabidhi baiskeli hizo, Mkurugenzi wa Secope, Antony Lyamunda, alisema kuwa matatizo wanayopitia shuleni hapo ni mengi, lakini kinachowaumiza wanafunzi ni umbali mrefu kutoka majumbani kwao kwenda shuleni.

Lyamunda alisema kuna vijana wanatoka umbali wa kilomita 11, hivyo kuwafanya watembee umbali wa kilomita 22 kila siku kwenda na kurudi.


"Mtoto anatembea umbali huo, lakini unaona shule inavyoendelea kufanya vizuri, shida inakuja madarasa ya mitihani kwa kuwa walimu wanakaa na watoto hadi jioni, hivyo lazima wanafunzi wafike usiku makwao, tumetoa hizi baiskeli kwa shule nzima huku tukimwomba Mungu tuweze kuanzisha ujenzi wa mabweni," alisema Lyamunda.

Kwa upande wake, mkuu wa shule hiyo, Henelieta Gosbert, alisema umbali mrefu wanaotembea wanafunzi kutoka majumbani kwenda shule ulikuwa unawakatisha tamaa baadhi ya wanafunzi.

Hata hivyo, Gosbert alisema mwamko wa wazazi umekuwa ni mkubwa hali inayowafanya wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani yao.

Mwalimu huyo alisema shule hiyo ina wanafunzi 125 wakiwamo wasichana 57 na wavulana 68, wakati 24 ndiyo wanatarajia kufanya mitihani ya kidato cha nne kwa mwaka huu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, Aidan Mhumpa, alisema msaada huo utapunguza kwa sehemu kubwa matatizo yaliyokuwa yanawakabili wanafunzi, lakini utaongeza muda wa vijana shuleni. Muhumpa aliagiza walimu kusimamia na kuzigawa baiskeli hizo kwa walengwa, ambapo kila mwanafunzi atakayemaliza shule ataikabidhi baiskeli shuleni kwa ajili ya kuwasaidia wengine watakaojiunga na shule.





Mfanyabiashara mdogo maarufu kama Machinga, akijipumzisha wakati akisubiri wateja katika eneo la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Radi yaleta maafa yaua mmoja, yajeruhi wawili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MMOJA amefariki dunia na wengine wawili wamenusurika kufa baada ya kupigwa na radi juzi majira ya saa nane mchana, huko katika kijiji cha Cheju Wilaya ya Kati Unguja.

Aliyefariki dunia ni Ayoub Uledi (18) mkaazi wa kijiji hicho, ambapo alifikwa na mauti hayo wakati akiwa amekaa chini ya mti.

Daktari katika Hospitali ya Mnazi Moja Zuleha Masoud, alisema kuwa kijana huyo alifikishwa hospitalini hapo akiwa tayari ameshafariki dunia baada ya kupigwa na radi.

Aidha, alisema pia alipokea majeruhi wawili ambao ni Punde Ayoub Uledi (16) ambaye ni ndugu wa marehemu aliyepigwa na radi na Mtumwa Suleiman Salum ambao wanaendelea kupatiwa matibabu katika hospitali hiyo.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Hassan, alisema kuwa majeruhi hao walipata mshtuko mkubwa kutokana na radi hiyo na hivi sasa hali zao zinaendelea vizuri.

Alieleza kuwa tayari mwili wa marehemu umeshakabidhiwa kwa jamaa zake kwa ajili ya mazishi na kuitaka familia hiyo kuwa na moyo wa subira.

"Hii ni mipango yake Mungu hakuna ambaye angependa kukutwa na mauti haya," alisema kamanda huyo.

Aidha, aliwataka wananchi wa mkoa huo kuchukua tahadhari hasa katika kipindi hiki cha mvua za masika zilizoanza kunyesha ili kuweza kuepukana na athari ambazo zinaweza kuepukika.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, alifika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwajulia hali majeruhi hao na kusema kuwa amepokea kwa mshtuko tukio hilo.

"Nimepokea kwa mshtuko mkubwa tukio hili la kusikitisha na mimi pamoja na wenzangu tulipata taarifa hizi tukiwa katika ziara ya kichama katika Mkoa wa Kusini Unguja na tumeamuwa kuja hapa ili kuwafariji," alisema.

# Balozi wa Ufaransa ahimiza kujifunza lugha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier, amewataka wananchi wa Zanzibar kujifunza lugha za mataifa mengine ikiwamo Kifaransa ili kuweza kuwasaidia katika harakati za kutafuta ajira.

Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa kituo cha utamaduni Mjini Zanzibar, kujua lugha za mataifa mengine ni muhimu hasa kwa maisha ya sasa hivyo wajitahidi kujifunza ili kupata fursa mbalimbali za kiuchumi na kiutalii.

Aidha, alisema kuwa mbali na kujifunza lugha za kigeni, lakini pia wasijisahau kujifunza na Kiswahili.

Frederic alisema Serikali ya Ufasansa itaisaidia Zanzibar katika kuendeleza utamaduni pamoja na kukuza lugha ya Kiswahili.

Alisema wataendelea kushirikiana na Serikali ya Zanzibar katika shughuli za ukuaji wa maendeleo hususan katika sekta ya elimu ili kuwawezesha vijana kuweza kujiajiri.

Akifungua kituo hicho, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, alisema Ufaransa imekuwa mdau muhimu katika kuimarisha maendeleo ya nchi, hivyo ni vyema wananchi wakaendelea kuthamini juhudi hizo.

Aliihakikishia Serikali ya Ufaransa kuwa wataendeleo kushirikiana katika kujifunza utamaduni kati ya nchi mbili hizo pamoja na kuulinda utamaduni ili uweze kuendelea kutoa fursa za ajira na kukuza utalii nchini.

Simai alimwomba balozi huyo kuwa mwakilishi mzuri wa lugha ya Kiswahili katika nchi yake ili hiyo iweze kuenea mataifa mengine.

Kwa upande wake rais wa kituo hicho cha utamaduni Said Khamis, alitoa wito kwa vijana kujiunga na kituo cha utamaduni kwa kuwa kinafundisha fani mbalimbali pamoja na lugha ya Kifaransa.

## Familia Tumbatu zanufaika mradi wa malezi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

FAMILIA zilizomo katika mradi wa malezi mbadala katika Kisiwa cha Tumbatu Kaskazini Unguja, zimesema kuwa tangu kuanza mradi huo maendeleo ya elimu kwa watoto wao yameimarika.

Wakizungumza na waandishi wa habari, familia hizo zimesema hivi sasa mahudhurio ya watoto wao shuleni ni mazuri ikilinganishwa na siku za nyuma, ambapo utoro ulikithiri.

Akizungumza kwa niaba ya familia hizo, Patima Ali Kona, alisema kuwa awali watoto wao walikuwa wakitoroka shule kutokana na hali ngumu ya maisha na kukaa na njaa kwa muda mrefu.

Alieleza kuwa watoto walikuwa wakienda shule bila ya kupata chakula wala fedha hali ambayo ilikuwa ikisababisha kushindwa kwenda shule.

Alisema tokea kuanza kwa mradi huo ambao umekuwa ukizisaidia familia zinazoishi katika mazingira magumu wamekuwa na uhakika wa kupata chakula angalau milo miwili kwa siku, ambapo kabla ya mradi huo walikuwa wakila mlo mmoja kwa siku.

"Hivi sasa tunashukuru watoto wanaenda shule wakiwa tayari wameshakula chakula au wakirudi shule wanakuta chakula cha mchana tayati, ambapo hapo awali mlo wetu ulikuwa ni nyakati za usiku tu," alisema.

Aidha, alieleza kuwa hali ya kukosa chakula kulitokana na hali ngumu ya maisha waliokuwa nayo na kulisababisha watoto wengi kuwa na utapiamlo.

Alieleza kuwa mradi wa malezi mbadala umewawezesha kuwapatia mtaji ya kufanya biashara ndogondogo na kupata fedha ambazo zinasaidia kwa ajili ya manunuzi ya chakula na mambo mengine.

Naye Namboto Khamis Shaame ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu kijijini hapo, alisema kuwa mradi wa malezi mbadala umemwezesha kufanya vizuri katika masomo yake na kufanikiwa kufaulu kidato cha pili na kuingia kidato cha tatu.

Alieleza kuwa mradi huo ulitoa elimu kwa familia zinazoishi katika mazingira magumu ikiwamo familia yake jinsi ya kuweza kuwalea watoto wa kuhakikisha wanapata haki zao ikiwamo haki ya elimu.

"Kwa kweli maisha yangu ya kielimu yalikuwa yanalega lega maana wakati mwengine siendi shule kutokana na njaa, lakini mradi huu uliiwezesha familia yangu na ikawa na ari na hamasa ya kunihimiza na kunifuatilia maendeleo yangu na matokeo yangu ya mtihani wa taifa wa kidato cha pili umeniwezesha kufaulu," alisema.

Kwa upande wake Shekha wa Shehia ya Tumbatu Uvuvini, Usi Khamis Nyange, alikipongeza kijiji cha kulelea watoto yatima SOS kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar (Tamwa), kwa kuendesha mradi wa malezi mbadala katika kisiwa cha Tumbatu.

Alieleza kuwa wananchi wa kisiwa hicho wanahitaji msaada mbalimbali kutokana na maisha yao kiuchumi ni magumu ikilinganishwa na maeneo mengine.

## HABARI KIMATAIFA

# Boeing yatangaza marekebisho ya ndege zake

**WASHINGTON,** Marekani

KAMPUNI ya Boeing imetangaza kufanya mabadiliko kwenye mfumo wa ndege unaozuia ajali.

Ndege za Boeing zimekuwa zikituhumiwa kuwa na hitilafu katika mfumo wa injini, baada ya kutokea kwa ajali mbili zilizosababisha vifo katika kipindi cha miezi mitano.

Baada ya kutokea kwa ajali hizo, nchi mbalimbali duniani zilizokuwa na ndege za Boeing zilisitisha safari kuhofia ajali zaidi.

Kama sehemu ya kuboresha ndege hizo, Shirika la Boeing limesema litaweka mfumo wa onyo kulingana na viwango, ambao awali ulikua si wa lazima.

Ndege za Boeing zilizopata ajali ni Lion Air ya Indonesia na Ethiopian Airlines, ambazo hazikuwa na mfumo wowote wa kuashiria ajali.

Shirika la Boeing lilisema lengo la mfumo huo ni kuwaonya marubani wakati mtambo wa uongozaji wa safari ya ndege unapotoa taarifa kinyume na matarajio.

Imesema nchi zilizonunua ndege aina ya Boeing hazitatoza pesa za ziada kwa ajili ya kuweka mfumo huo wa usalama wa ndege. Pia watafanyia mabadiliko programu ambayo imehusishwa na ajali.

Mfumo huo uitwao MCAS uliundwa kuzuwia ndege kupoteza mwelekeo huwa unatambua taarifa za kifaa pindi ndege ikiwa katika mwinuko wa kasi wa kupindukia au la.

Lakini uchunguzi wa ajali ya ndege ya Lion Air iliyotokea mwaka jana ulionyesha kuwa mfumo huo ulikuwa haufanyi kazi na kulazimisha ndege kuelekea chini zaidi ya mara 20 kabla ya kuanguka ndani ya bahari na kuwauwa abiria 189 pamoja na wahudumu.

Katika taarifa iliyotolewa kwa waandishi wa habari jana, Boeing ilisema kuwa kubadilishwa kwa mfumo wa usalama wa ndege zake hakumaanishi kukiri kuwa mfumo uliokuwapo ulisababisha ajali. **BBC**



Wakazi wa kijiji cha Praia Nova, nchini Msumbiji wakiendelea na shughuli zao, kwa sasa wakazi hao wamerejea katika makazi yao baada ya kimbunga Idai kuikumba nchi hiyo. **PICHA: REUTERS**

# Wabunge Uingereza wapinga mapendekezo ya Waziri Mkuu

**LONDON,** Uingereza

BUNGE la Uingereza limepinga mapendekezo yote yaliyotolewa kama mbadala kwa mpango wa Uingereza kujitoa kwenye Umoja wa Ulaya ujulikanao kama Brexit, na Waziri Mkuu, Theresa May.

Bila ya mpango mpya Uingereza italazimika kuondoka EU bila ya mkataba ifikapo Aprili 12.

Mapendekezo hayo ni kuondoka Umoja wa Ulaya bila mkataba, kubakia katika umoja wa forodha na soko la pamoja la jumuia hiyo, kuitisha kura ya maoni juu ya mkataba wowote utakaofikiwa, kuubatilisha mchakato mzima wa Brexit kama hakuna matarajio ya kufikia makubaliano.

Waziri Mkuu May alisema angejiuzulu ikiwa mpango wake wa Brexit utapitishwa na wabunge.

Akizungumza kwenye mkutano wa chama chake, May aliwaambia wabunge kwamba atajiuzulu kabla ya hatua ya pili ya mazungumzo kuanza.

Hatua hiyo ya Waziri Mkuu May ni jitihada za mwisho za kutafuta washirika wa kutosha ili kuunga mkono mpango wake mpya anaotarajia kuuwasilisha bungeni kwa mara ya tatu baada ya kukataliwa mara mbili.

May anakabiliwa na shinikizo linaloongezeka kutoka kwa wabunge wanaounga mkono mchakato wa Brexit katika chama chake, ambapo wanamtaka aachie madaraka.

May analaumiwa kujadili mpango mbovu wa Brexit utakaoifanya Uingereza isiwapo EU.

Waziri wa mambo ya Nje wa zamani wa Uingereza, Boris Johnson alitangaza kuwa atauunga mkono mpango wa May ambao awali aliuita ni wa kudhalilisha.

Kuna uwezekano mkubwa Johnson ndiye atakayechukua nafasi ya uwaziri Mkuu endapo May akijiuzu.

Wakati huo huo, chama cha Democratic Union (DUP) cha Ireland ya Kaskazini kinachoiwezesha serikali ya May kuwa na viti vingi bungeni kimesema kwamba kitaupinga mpango wa Waziri Mkuu.

Matokeo yaliyotoka yanaweza kuifanya Uingereza iendelee kukwama kiuchumi katika EU hatua ambayo itailazimu nchi hiyo iombe muda zaidi kabla ya kujiondoa.

Mjumbe mkuu wa EU katika suala la Brexit, Michel Barnier alikutana jana na wajumbe kutoka nchi wanachama 27 wa UE mjini Brussels.

Wajumbe hao walijadili hatua zinazofuata baada ya wabunge wa Uingereza kupiga kura juzi.

Naye Rais wa Baraza la Ulaya, Donald Tusk alisema EU unapaswa kuiruhusu Uingereza kushiriki kwenye uchaguzi wa bunge la Ulaya ikiwa itaashiria kwamba itabadili mchakato wa kujiondoa.

Alisisitiza kwamba EU hautawasaliti mamilioni ya Waingereza ambao wanataka kubakia kwenye junuiya hiyo. **DW**

## Kipindupindu chapiga hodi Zimbabwe

**HARARE,** Zimbabwe

BAADA ya Zimbabwe kukumbwa na kimbunga Idai na kusababisha mafuriko katika miji kadhaa, Wananchi wa nchi hiyo kwa sasa wanakabiliwa na ugonjwa wa kipindupindu.

Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) limetuma dozi 900,000 kama chanjo ya ugonjwa wa Kipindupindu nchini humo.

Watalaam wa afya wameonya kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutokea madhara zaidi kwa magonjwa mengine kutokea mbali na kipindupindu kutokana na kimbunga kilichotokea nchini humo wiki iliyopita na kusababisha mamia ya watu kupoteza maisha na maelfu kuyakimbia makazi yao.

Tayari watu watano wamethibitishwa kuambukizwa ugonjwa huo, hata hivyo baadhi ya watu wameanza kurejea katika baadhi ya maeneo hususani katika kijiji cha Praia Nova.

Hii ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazokabili mji wa Beira katikati ya Msumbiji, maeneo ambayo yaliathiriwa zaidi na Kimbunga Idai.

Imekuwa ni vigumu kudhibiti maelfu ya tani ya takataka ambazo kimbunga hicho kimesababisha.

Mji wa Beira umetenga maeneo matatu ili kupokea takataka hizo zote, mojawapo ya maeneo hayo ni eneo la Ceramica uliopo kilomita 20 kutoka Beira. **RFI**

## Museveni akutana na Kenyatta, wazungumzia biashara

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amezuru Kenya kwa ziara ya siku mbili na kukutana na mwenyeji wake Rais Uhuru Kenyatta Ikulu ya Mombasa kwa mazungumzo.

Viongozi hao wamezungumzia masuala ya biashara kati ya nchi hizo mbili za Afrika Mashariki, wakati huu Uganda ikiendelea kuvutana na Rwanda kuhusu masuala ya kibiashara.

Jana Rais Museveni alitarajia kuzuru Bandari ya Mombasa ambayo Uganda inatumia kupokea idadi kubwa ya mizigo yake.

Katika hatua nyingine, Rais Kenyatta alisema amekubaliana na mwenzake kuhusu namna ya kutatua mzozo wa kisiwa cha Migongona na namna ya kunufaika na maji ya Ziwa Victoria. **RFI**

# Takukuru kuanzisha dawati maalumu la rushwa ya ngono

**Na Jumbe Ismailly,** MKALAMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (Takukuru), inatarajia kuanzisha dawati maalumu la kushughulikia rushwa ya ngono katika ofisi zake zote pia litakuwa na jukumu la kuelimisha na kuuhamasisha zaidi umma kuwa na ujasiri wa kutoa taarifa na kupinga vitendo vya rushwa ya ngono.

Ofisa Uchunguzi wa Takukuru wilaya ya Iramba na Mkalama Benjamin Masyaga, aliyasema hayo wakati akitoa mada kwenye mkutano mkuu wa nane wa Chama cha Makatibu Mahususi (TAPSEA), Mkoa wa Singida uliofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Alisema kupitia dawati hilo, litasaidia kupunguza au kuondoa kabisa kero hiyo ambayo kwa kiwango kikubwa inawaathiri wananchi wa jinsia ya kike.

Kwa mujibu wa Masyaga katika siku za hivi karibuni zimeibuliwa tuhuma nyingi katika jamii zinazohusu rushwa ya ngono zilizoambatana na matukio ya Takukuru kuwakamata waliodaiwa kuomba rushwa ya ngono.

Alisisitiza pia katika kipindi cha mwaka 2015 - 2018 taasisi hiyo imepokea na kufanya uchunguzi dhidi ya malalamiko tisa yanayohusu rushwa ya ngono na kati ya tuhuma hizo, kesi tano zilishafikishwa mahakamani na kutolewa hukumu.

"Kufuatia matukio hayo na kwa kutambua mchango wa makatibu mahususi, katika kuliletea taifa letu maendeleo na kupambana na rushwa, kuanzia sasa Takukuru itakuwa na dawati maalumu litakaloshughulikia rushwa ya ngono katika ofisi zake zote na kupitia dawati hili tutaelimisha na kuuhamasisha zaidi umma kuwa na ujasiri wa kutoa taarifa na kupinga vitendo vya rushwa ya ngono," alifafanua.

Aidha, alisisitiza kwamba taasisi hiyo inachukua fursa hiyo kutamka kuwa inaunga mkono juhudi zinazoendelea mkoani Singida za kuhakikisha makatibu mahususi wanalindwa na inapinga unyanyasaji na udhalilishaji wa aina yoyote unaofanywa dhidi ya makatibu mahususi, ikiwamo kulazimishwa kutoa rushwa ya ngono.

Awali akimkaribisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Geofrey Sanga, Mwenyekiti wa TAPSEA Mkoa wa Singida, Elizabeth Msing'ha aliwataka makatibu mahususi kutumia muda wao vizuri kwa kufanyakazi kwa ufanisi na kuleta tija kazini.

Aidha, alisisitiza kaulimbiu yao ya kutumia muda wao vizuri kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija kazini na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.

Akifungua mkutano huo, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Mkalama, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Fredy Kimeme, alitoa wito kwa waajiri wote wa umma na binafsi kuwekeza katika teknolojia mpya zinazoingia kila wakati, pia katika ujuzi na ufahamu wa watumishi wanaotumia teknolojia hizo ili waweze kutoa huduma bora kama ilivyotarajiwa.

Alisema teknolojia itakuwa na maana pale itakapotumiwa na watu walio na maarifa kwa kuwa bila maarifa teknolojia haiwezi kusaidia chochote.




Mwakilishi wa BancABC, Emmanuel Nzutu, akikabidhi msaada wa mabati kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Sauda Mtondoo, juzi wilayani humo. **MPIGAPICHA WETU**

## TCRA: Watumiaji simu uelewa mdogo

**Na Mary Geofrey**

WAKATI Teknolojia ya Mawasiliano ikikua kwa kasi nchini, uelewa mdogo wa watumiaji na wamiliki wa simu za mkononi umekuwa changamoto kubwa.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi James Kilaba, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alikuwa akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa Wadhibiti wa Jukwaa la Sekta ya Mawasiliano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (Sadec).

Alisema vikwazo vilivyo katika sekta ya mawasiliano nchini vinatokana na kasi ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano hali inayosababisha matumizi mabaya ya simu kutokana na uelewa mdogo.

"Tenkolojia ya mawasiliano inakua kwa kasi sana na kikwazo kikubwa ni watu kukosa uelewa wa namna ya kutumia vifaa vya mawasiliano na matokeo yake kusababisha makosa ya matumizi ya mitandao kama vile mtu kujipiga picha na kuituma bila ya yeye kufahamu kama ametuma," alisema Kilaba.

Alisema mkutano huo utajadili namna ya kufikisha mawasiliano maeneo ya vijijini.

Kilaba alisema mkutano huo unatoa fursa ya kujifunza, kuweka uwiano katika tozo ya mawasiliano na usalama wa mitandao, miundombinu na watumiaji.

"Tanzania imekuwa nchi ya mfano katika sekta ya mawasiliano na nchi zingine wanajifunza kutoka kwetu kwa lengo la kuboresha sekta hiyo katika nchi za Sadec," alisema.

Akifungua mkutano huo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashanta Nditiye, alisema wanajadili namna ya kuchukua tahadhari na kuzuia uhalifu wa matumizi ya mitandao.

Alisema pia nchi zinazoshiriki mkutano huo zinashirikiana kuangalia namna ya kupunguza tozo za kupiga simu ili wananchi wake wanufaike na sekta ya mawasiliano pamoja na huduma za utoaji mawasiliano kwa njia ya redio.

Kuhusu gharama za mawasiliano nchini, Nditiye alisema ni ndogo kulinganisha na nchi zingine kwa sababu wamefanikiwa kusambaza mikongo ya mawasiliano maeneo mengi nchini.

Alisema gharama za kupiga simu mtandao mmoja kwenda mwingine ni Sh. 10 na senti 50, jambo linalowapunguzia mzigo wananchi kutembea na simu nyingi za laini tofauti.

# Kutukana wanawake sokoni faini 15,000/-

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SOKO Kuu la Shinyanga Mjini limetunga na kupitisha sheria ndogo kuwa mfanyabiashara ambaye atatoa lugha chafu za matusi, atalipa faini shilingi 15,000.

Mbali na kulipa kiasi hicho cha fedha, mhusika pia atapewa adhabu ya kutofanya biashara kwa wiki mbili au vyote kwa pamoja.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa soko hilo, Alex Stephen, wakati akichangia mada kwenye semina ya viongozi wa masoko sita ya mjini hapa. Washiriki wengine ni mgambo, watendaji wa kata, dawati la jinsia, askari polisi pamoja na maofisa maendeleo, lengo likiwa kutokomeza ukatili wa kijinsia katika masoko.

Alisema ili ukatili wa kijinsia sokoni ukome, ni lazima kujiwekea sheria ndogo, ambayo itakuwa ikiwabana wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiendekeza vitendo vya ukatili, ikiwamo utoaji wa lugha chafu za matusi ya nguoni na kuwadhalilisha wanawake.

"Kwenye soko letu baada ya kuona ukatili wa kijinsia unazidi hasa utoaji wa matusi ya nguoni, ndipo tukaona tutunge sheria ndogo ambayo itatusaidia kukomesha vitendo hivi," alisema na kuongeza:

"Mpaka sasa imetusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukatili dhidi ya wanawake."

Naye Katibu wa Soko la Kambarage, Maria Mauki, alisema na wao wameshatunga sheria ndogo na kuipitisha, kuwa mfanyabiashara ambaye atabainika kufanya ukatili wa kijinsia kwa kutoa lugha za matusi, kumpapasa mwanamke ama kumtaka kimapenzi kwa nguvu, atapigwa faini ya Sh. 5,000, na kutofanya biashara miezi mitatu.

Mtoa mada ambaye ni mwanasheria wa kujitegemea, Matha Masalu kutoka Kampuni ya Masalu Law Attorneys mkoani Shinyanga, alisema ukatili wa kijinsia ni kosa chini ya sheria ambayo inazuia mwanamke kutolewa lugha chafu za matusi, pamoja na kushikwa shikwa sehemu zake za siri.

Ofisa mradi huo wa kutokomeza ukatili wa kijinsia katika masoko, Mustapha Isabuda, kutoka Shirika la Agape la kupinga ukatili kwa watoto na wanawake mkoani Shinyanga, alisema utatekelezwa kwa mwaka mmoja ili kumaliza kabisa vitendo vya ukatili kwenye masoko.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## *NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BEATRICE PASTORY SILAYO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya T/HIACE yenye namba za usajili T 589BAD Chassis namba LH174000724.Engine NO.5L5091996.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/508/2019.**

xxxxxx

### ENEO/KIWANJA KINAUZWA

**Eneo/kiwanja kinauzwa Tshs mil 150.Kipo** Tabata Segerea barabarani, kina ukubwa wa mita za mraba 2690. Kina hati na nyaraka zote miliki,kinafaa kwa matumizi ya biashara kama Shule,Yadi, kituo cha mafuta.n.k.

**KWA MAWASILIANO: 0759974831 / 0693410359. OWNER**

115146002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENNY RUMISHAEL MAKUNDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 662 BRY MITSUBISHI FUSO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RHE/RB/435/2019.**

215144802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1994 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: TEMEKE

Usimamizi wa Mirathi No. 111/2019
Ombi la **DADI AHMEDI MAGWAYA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu ZUBED JUMA ILAMBA.

Kwa: **MHARIRI WA GAZETI LA NIPASHE**
**DSM-TANZANIA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 10/4/019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizii wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 26/3/2019

115144602

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.25 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late REGINA NYAMKAKALO MUSIBA**

**In the matter of Application for letters of Administration by CRISPIN C. MUSIBA**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before **17TH /04/2019.**

Dated at Dodoma this ….28 /03/2019

215145902

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.27 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late**
**DINA MAKAMILO LISASI**

**AND**

**In the matter of Application for letters of Administration AIDAN MARTIN CHALLO**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of probate for letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 24TH /04/2019.

Dated at Dodoma this ….27 /03/2019

115145101

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ERASMO WALTER MWAGENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 111 CAP TOYOTA ALTEZZA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TUN/RB/612/2019.**

215144702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JONAS MODEST ITEMBA,** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 751 APF SUZUKI.** Chassis namba TDO1W117333 na injini namba G 16A254536.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **MOS/TR/RB/573/2019.**

115145202

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GEEZ TRADING COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 382 BXD SUZUKI CARRY. Chassis namba DA52T224620. Engine namba F6AEAA4620.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KMR/RB/3134/2019.**

115145802

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Joyce D. Mariki** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T372 CHD aina ya SUZUKI ESCUDO, yenye chasis namba TD0IWI01502, Engine namba 616A208066.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: OB/RB/2935/2019**

115145702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ROMUALD GOSBERT NGEIYAMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 364 AAK NISSAN DATSUN. Chassis namba **QD21423125.** Engine namba 20003218.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **BU/TR/RB/123/2019.**

115145502


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***
***Tupigie 0767 223 311***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SANE kupewa mkataba mpya

**MANCHESTER,** England

WINGA wa Manchester City, Leroy Sane, anaweza kulipwa mshahara mkubwa zaidi wakati mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England wakiwa wameanza majadiliano ya kumpatia mkataba mpya.

Akiwa amebakiwa na miaka miwili katika mkataba wake wa sasa, Sane amekuwa katika majadiliano ya mkataba mpya hasa baada ya nyota kama, Raheem Sterling, Gabriel Jesus na Sergio Aguero wote wakiwa wamesaini mikataba ya muda mrefu.

Gazeti la The Mirror limesema kwamba klabu hiyo inataka kumpa mkataba wa miaka mitatu na mshahara wake utaongeza mara mbili kutoka anaolipwa sasa wa pauni 180,000 kwa wiki.

Sane amekuwa katika kipaji kizuri tangu atue hapo mwaka 2016 akitokea Schalke kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 36.

Licha ya kuwa kwenye wakati mgumu mwanzoni mwa msimu, amejiimarisha na kuwa kwenye kikosi cha kwanza chini ya kocha Pep Guardiola, na amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho 17 kwenye mechi 38 msimu huu.

Alikuwa pia katika orodha ya wafungaji wakati City wakiifunga Schalke mabao saba na kufuzu hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na kiwango chake kimemfanya kuitwa tena katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Ujerumani baada ya kutemwa kwenye michuano ya Kombe la Dunia.

Na aliifungia bao Ujerumani wakati ikiibuka na ushindi wa magoli 3-2 dhidi ya Uholanzi Jumapili iliyopita.




## Madrid kumkabidhi mamilioni Zidane

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imepanga kumpa kocha wake mpya, Zinedine Zidane euro milioni 500 kwa ajili ya kufanya usajili.

Fedha hizo amepewa ili kuweza kuwasajili wachezaji kama Kylian Mbappe, Eden Hazard na Paul Pogba katika miezi inayokuja.

Zidane aliondoka klabuni hapo baada ya kuiwezesha kutwaa mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Lakini baada ya nafasi yake kuchukuliwa na Julen Lopetegui ambaye alitimuliwa na Santiago Solari akachukua mikoba yake naye alitimuliwa na Zidane kupewa tena nafasi hiyo.

Kumekuwa na uvumi kwamba wachezaji 18 wamekuwa wakihusishwa na kujiunga na timu hiyo ambao ni mapendekezo ya Zidane.

Habari zaidi zinasema kwamba, baada ya Madrid kupata mapato ya euro milioni 751 msimu uliopita, Rais Florentino Perez ameshawishika kutoa kiasi hicho cha fedha ili kuleta nyota wapya.

Mbappe anatajwa kwamba ana thamani ya euro milioni 280 kwa ajili ya kumsajili akiwa amefunga mabao 31 katika mechi 35 alizoichezea Paris Saint-Germain.



## Barca yataja thamani ya Malcom

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imetaja kiasi cha euro milioni 70 kwa timu yoyote itakayomtaka winga wa kimataifa wa Brazil, Malcom (pichani chini).

Malcom ametajwa kuwa anaweza kuondoka hapo kwenye dimba la Camp Nou, huku klabu za Inter, Arsenal na Tottenham zikitajwa kumwania mchezaji huyo.

Barca ilitumia euro milioni 41 kumsajili Malcom kutoka Bordeaux kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 hajawa kwenye kiwango kizuri chini ya kocha, Ernesto Valverde.

Kutokana na kushindwa kupata nafasi ya kucheza, Barca sasa imeamua kumuuza mchezaji huyo.

Gazeti la Marca limedai kuwa thamani ya Mbrazil huyo ni euro milioni 70.

Malcom ameshinda kabisa kupenya kwenye kikosi cha kwanza, kwa kuwa hajaanza katika mchezo wowote wa La Liga tangu Novemba mwaka jana.

Amecheza dakika 32 tu kwenye Ligi Kuu tangu kuanza kwa mwaka huu na hakutumika katika mechi sita wakati akiwa benchi.



## HABARI MICHEZO

# Chelsea wampeleka Hudson-Odoi kwa mwanasaikolojia

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kuwa katika mipango ya kumpeleka kwa mwanasaikolojia nyota wake, Callum Hudson-Odoi (pichani chini), kutokana na mchezaji huyo kukumbwa na changamoto za ubaguzi wa rangi akiwa na timu yake ya Taifa ya England.

Callum mwenye umri wa miaka 18 atafanyiwa ushauri nasaha, baada ya kujikuta katika wakati mgumu wa kubaguliwa kutokana na rangi ya ngozi yake akiwa katika klabu yake ya Chelsea na England, kwa nyakati mbili tofauti.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Hudson- Odoi atapewa ushauri nasaha na mwanasaikolojia kwa muda wa wiki mbili.

Mchezaji huyo kinda wa Chelsea alikutana na tukio la kibaguzi akiwa na wachezaji wenzake wa England, Raheem Sterling na Danny Rose wakiwa katika mchezo wa kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Montenegro, mchezo ambao ulimalizika kwa England kushinda mabao 5-1.

Kutokana na kitendo hicho kilichofanywa na mashabiki wao kuwaita wachezaji wa England kama nyani, Montenegro tayari wamefunguliwa shtaka na UEFA na litasikilizwa Mei 16, mwaka huu na kama watakutwa na hatia ya kutenda kosa hilo, adhabu yao ya chini kabisa inaweza kufungiwa kuingiza idadi ya mashabiki wengi uwanjani.






# VAN GAAL ajibu tuhuma za Di Maria

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal, amejibu tuhuma za Angel Di Maria dhidi yake.

Van Gaal ambaye aliamua kustaafu jumla kazi ya kufundisha soka tangu alipofukuzwa kazi United kwa sababu za kiwango cha timu hiyo kutowaridhisha mabosi wa klabu hiyo, amesema Di Maria alishindwa kumshawishi.

Di Maria ambaye hakuwa na mahusiano mazuri na Van Gaal na baadaye kutimkia katika Klabu ya Paris Saint Germain ya Ufaransa, alidai kuwa kocha huyo ndiye aliyesababisha yeye kuondoka hapo.

Nyota huyo alisema kwamba, Van Gaal alikuwa haonyeshi kumkubali na ndicho kilichofanya hata asirudi tena United wakati wa maandalizi ya msimu hadi anahama.

Akihojiwa na BBC, Van Gaal amejibu yote na Di Maria alishindwa kuonyesha kiwango na hakumshawishi.

"Anasema mimi ndio nilikuwa tatizo? Nilimpanga katika nafasi zote za ushambuliaji, lakini hakunishawishi katika nafasi zote hizo.

"Hakuweza kunishawishi na kuonyesha kiwango chake na hivyo nikaona hanifai kwa sababu mimi nilikuwa nataka matokeo uwanjani, lakini yeye hakuwa katika kiwango chake.

"Alishindwa kukabiliana na mfululizo wa presha ya Ligi Kuu England na mimi sikuwa na jambo jingine la kufanya juu yake."



# Mama wa Rabiot ailalamikia PSG

**PARIS,** Ufaransa

MAMA mzazi wa mchezaji wa Paris Saint Germain, Andrien Rabiot ambaye pia ni wakala wake, Veronique Rabiot amedai kuwa mtoto wake anafanywa kama mfungwa kwenye klabu hiyo.

Veronique amesema kuwa namna ambavyo anachukuliwa mwanaye ni tofauti na wanavyochukuliwa baadhi ya wachezaji wa timu hiyo, kitu ambacho ameweka wazi kwamba hafurahishwi nacho hata kidogo.

Mkataba wa Rabiot unamalizika mwisho wa msimu huu na ameweka wazi msimamo wake kuwa hatoendelea nao.

Uamuzi wa Rabiot kutoendelea kuichezea PSG umesababisha nyota huyo atolewe katika orodha ya wachezaji wanaotakiwa kufanya mazoezi na kikosi cha kwanza.

Hata hivyo, mama yake amelalamika kuwa mwanawe na baadhi ya wachezaji hawapewi usawa na amekuwa akipendelewa zaidi Neymar kufanya anachotaka kama sasa hivi ni majeruhi lakini alionekana katika matamasha ya usiku.

"Mwanangu ni kama mfungwa PSG kitu pekee alichoomba ni kumalizia mkataba wake, walimpiga faini kwa sababu ya kutosafiri na timu kwenda Qatar wakati ambao alikuwa kafiwa na bibi yake," amesema.

"PSG wamekuwa na utamaduni wa kuwapiga faini wachezaji wanaochelewa katika kikao kwa dakika sita, lakini wengine wakiwa majeruhi (Neymar) wanaruhusiwa kusafiri mahala popote duniani kuhudhuria matamasha."

PSG iliwapiga faini ya euro 180,000 Kyliane Mbappe na Andrien Rabiot kama sehemu ya kuwaadhibu na kuwapa onyo kufuatia kitendo chao cha uchelewaji katika kikao cha timu Oktoba 2018.



## KWA UFUPI

### HUDSON-ODOI: NITAONDOKA
WINGA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi, amesema anataka kuondoka mapema katika klabu hiyo na hataki kupoteza nafasi zilizojitokeza, huku tayari Barcelona na Manchester United zikiungana na Bayern Munich kuwania saini yake. **(Mail)**

### DORTMUND: SANCHO HAUZWI
MABOSI wa Borussia Dortmund wamesema hawana mpango wa kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19), ambaye anahusishwa na mipango ya kujiunga na Manchester United. **(Mirror)**

### UNITED YAJIPANGA SOKONI
JADON Sancho na kiungo wa West Ham na England, Declan Rice (20), wako katika nafasi ya juu katika orodha ya nyota wanaotakiwa na Manchester United katika kipindi cha majira ya joto, pamoja na beki wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka (21). **(Sun)**

### BARCA WAITEGA UNITED
BARCELONA inajiandaa kuipa Manchester United mchezaji wake, Philippe Coutinho (26) au Malcom (22) kama sehemu ya kufanikisha mchakato wa kumsajili straika wa England, Marcus Rashford (21) kutua Nou Camp. **(Mundo Deportivo, via Mail)**

### FODEN AJIPANGA CITY
KIUNGO wa Manchester City, Phil Foden (18), anatarajia kusitisha ofa za kuelekea Ujerumani kwa ajili ya kuhakikisha anapata namba katika kikosi cha kwanza cha timu ya Pep Guardiola. **(Mail)**

### LEICESTER YAKATA TAMAA
LEICESTER City imetoa msimamo kuwa nyota wake anayetakiwa na Manchester United, Harry Maguire (26) na beki wa England, Ben Chilwell (22) ambao wanahusishwa na mpango wa kujiunga na Manchester City kuwa hawauzwi. **(Mirror)**

### DE GEA, UNITED BADO
NAFASI ya Manchester United kushiriki mashindano yajayo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya bado iko katika hatihati kutokana na mazungumzo yanayoendelea ya kusaini mkataba mpya na golikipa wake Mhispania, David de Gea (28). **(Manchester Evening News)**

### UNITED: SANCHEZ HAUZWI
KLABU ya Manchester United imesema haina mpango wa kumuuza nyota wake anayelipwa mshahara mkubwa, Alexis Sanchez (30), licha ya kuwa bado iko katika mazungumzo na golikipa wake Mhispania, De Gea kwa ajili ya kusaini mkataba mpya. **(London Evening Standard)**

### UNITED: HERRERA ATABAKI
MANCHESTER United imesema kuwa inaamini kiungo wake Mhispania, Ander Herrera (29), ambaye anatarajia kumaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu, atasaini mkataba mpya licha ya kutakiwa na Arsenal na Paris St-Germain.**(Metro)**

### LOVREN ANG'ARA SOKONI
BEKI wa Liverpool, Dejan Lovren, ameanza kuwindwa na Roma, Napoli na AC Milan katika kipindi cha usajili cha majira ya joto. **(Mirror)**

### JAMES AGOMBEWA
MANCHESTER City imetajwa kuwa ni moja ya klabu zilizojitokeza kumwania winga wa Swansea na Timu ya Taifa ya Wales, Dan James ambaye ana umri wa miaka 21. **(Sun)**

### GRUJIC ANOGEWA UJERUMANI
KIUNGO wa Liverpool Mserbia, Marko Grujic, ambaye yuko kwa mkopo katika Hertha Berlin, amesema kuwa anataka kubakia katika klabu hiyo ya Ujerumani kwa mwaka mwingine mmoja. **(Liverpool Echo)**

### SANTON AJIVUNIA NEWCASTLE
BEKI wa zamani wa Newcastle, Davide Santon (28), ambaye yuko kwa mkopo Roma, amesema kuwa Magpies itaendelea kuwa kwenye moyo wake na kocha Rafael Benitez amefanikiwa kuendelea kukuza kipaji chake. **(Chronicle)**

DO OOO OKA
M ZETI AYA



# NDOTO ZA SOLSKAJER ZATIMIA

## ● ● ● Ni baada ya United kumpa rasmi mkataba wa kudumu wa kuifundisha timu hiyo...

**MANCHESTER,** England

HATIMAYE Ole Gunnar Solskjaer amesaini mkataba wa kudumu wa miaka mitatu wa kuifundisha Manchester United baada ya kupata mafanikio katika kipindi chake akiwa kocha wa muda.

Kocha huyo raia wa Norway, amerejea Old Trafford Desemba mwaka jana, na amepewa mkataba huo baada ya kupata baraka kutoka kwa familia za Ed Woodward na Glazer kutokana na kuiongoza timu hiyo kushinda mechi 14 kati ya michezo 19 iliyocheza.

Imebainika kuwa Solskjaer alipewa mkataba huo wa kudumu mapema wiki hii baada ya kukutana uso kwa uso na Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa klabu hiyo, Woodward alipokutana naye kwenye viwanja vya mazoezi.

Mkataba wake una thamani ya pauni milioni saba kwa mwaka, pungufu ya nusu ya pauni milioni 18 ambazo klabu ilitumia kumlipa aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Jose Mourinho.

Sportsmail pia linafahamu kuwa United italazimika kuilipa kiasi cha fedha ambacho hakijawekwa wazi, lakini ikiwa na tarakimu sita, klabu ya zamani ya Solskjaer iitwayo Molde. Hili halina mjadala, ni malipo ambayo lazima yatatekelezwa na klabu hiyo ya Old Trafford kutokana na makubaliano ya amani.

Tayari Solskjaer alikuwa ameshaanza kujipanga kuhusu uhamisho wa wachezaji katika kipindi cha majira ya joto ikiwa ni mipango ya muda mrefu.

Fungu kwa ajili ya mchakato huo lilishaandaliwa na taarifa kutoka kwa vyanzo vya klabu hiyo zinasema kuwa sasa mchakato huo itaelekea kukamilika.

Solskjaer alipata ushirikiano mkubwa ndani ya timu hiyo tangu alipotua kutoka kwa wachezaji nyota ambao ni pamoja na Paul Pogba, Marcus Rashford na Anthony Martial.

"Kuanzia siku ya kwanza niliyotua, nilijisikia niko nyumbani, hii ni klabu maalumu kwangu," alisema Solskjaer alipohojiwa na mtandao wa klabu hiyo.

"Ilikuwa ni jambo ya heshima kuwa mchezaji wa Manchester United na kuanza kazi ya ukocha hapa. Kwa kipindi cha miezi michache niliyokaa hapa nilijifunza vitu vizuri na ninataka kuwashukuru makocha, wachezaji na wafanyakazi wote ambao nimefanya nao kazi hapa kwa sasa.

"Kazi hii nilikuwa ninaiwaza na ilikuwa kwenye ndoto zangu na nimefarijika kufanikiwa kupata nafasi hii ya kupata mkataba wa muda mrefu na ninaamini nitaendelea kuwapa mafanikio ambayo mashabiki wanastahili kuyapata."

Kocha huyo alikuwa ni mchezaji wa zamani wa timu hiyo kati ya mwaka 1996 na 2007, akifunga mabao 126 katika mechi 366 alizocheza.

Baada ya hapo alianza kukifundisha kikosi cha akiba cha timu hiyo mpaka mwaka 2011, na alifanikiwa kurejesha furaha iliyopotea baada ya kuwa na wakati mgumu chini ya Mourinho.

## HABARI MICHEZO

# AZAM, KAGERA SUGAR HAPATOSHI KAITABA LEO

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA wa Azam FC, Iddi Cheche na Mecky Maxime wa Kagera Sugar, ambao wanakutana katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya Kombe la FA, kila mmoja anakihofia kikosi cha mwenzake, imefahamika.

Kagera Sugar inatarajia kuikaribisha Azam FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Cheche aliliambia gazeti hili kuwa amekwenda Bukoba na kikosi kamili kwa sababu anafahamu mchezo huo utakuwa na ushindani kutokana na kila timu kuhitaji kuchukua kombe hilo.

Alisema uzoefu wa wachezaji wa Kagera Sugar unamfanya kukipanga zaidi kikosi chake na kuongeza umakini katika mchezo huo.

"Kagera Sugar ni wazoefu katika ligi na mashindano mengine mbalimbali, nakumbuka wao ndio wenyeji wa mechi hii, tunatarajia kukutana na ushindani, kwa kifupi tumejipanga kusaka matokeo mazuri," alisema Cheche.

Aliongeza kuwa wameamua kuwekeza nguvu zaidi katika mashindano hayo kwa sababu wanahitaji kupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho hapo mwakani.

Maxime alisema hana hofu ya kuwakabili Azam FC, lakini anafahamu wazi mchezo huo utakuwa na upinzani kama walivyokutana katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tulianza maandalizi mapema kwa ajili ya kuhakikisha tunasonga mbele katika mashindano haya ya Kombe la FA, hii ndio nafasi pekee ambayo inaweza kutupeleka katika michuano ya kimataifa mwakani, kila mmoja anatizama hapa," alisema Maxime.

Baada ya mechi ya leo, Azam FC itaikaribisha Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Aprili 3, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.



Wachezaji wa Simba, Jonas Mkude (kulia) na Haruna Niyonzima wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbao FC itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro. **PICHA: SSC**

## Singida yafunguka 'kilichowaua' Bara

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Singida United imesema kuwa moja ya sababu zilizochangia timu yao kufanya vibaya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA msimu huu, ni kusajili wachezaji kutoka Simba na Yanga.

Kauli hiyo ya Singida United imekuja siku moja baada ya kufungwa mabao 2-0 na Lipuli FC na kuondolewa katika mashindano ya Kombe la FA ambayo yanaendelea hapa nchini.

Mkurugenzi wa Singida United alisema jana kuwa kusajili nyota wanaotoka Simba na Yanga, ndio walioanzisha migogoro ndani ya timu yao ambayo msimu huu imekuwa pia ikikabiliwa na changamoto ya ukata.

Sanga alisema kuwa nyota hao wamekuwa wakishindwa kuwajenga wachezaji chipukizi pale klabu inapokuwa na hali mbaya kiuchumi au kushindwa kutekeleza malipo ya mishahara kwa wakati.

"Kufanya vibaya kwa timu yetu kumetokana na kusajili wachezaji wengi kwa gharama kubwa, gharama hizo zimefanya kwa sasa tushindwe kuzimudu na kujikuta tukiiendesha timu kwa tabu," alisema Sanga.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Singida United iko katika nafasi ya 18 ikiwa na pointi 33 baada ya kushinda mechi nane, sare mara tisa kati ya michezo 30 waliyocheza.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Ukata waitesa Twiga Stars

**Na Mwandishi Wetu**

HALI ya ukata imekuwa ni moja ya changamoto zinazoikabili timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) ambayo inajiandaa kuwakaribisha wenzao wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) katika mchezo wa kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki utakaochezwa Aprili 5, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Timu hizo zitarudiana baada ya siku nne mjini Kinshasa na mshindi atasonga mbele.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema kuwa wachezaji wake wako katika hali nzuri na mazoezi lakini bado hajafanikiwa kupata mechi za kirafiki.

Shime alisema kuwa kutokana na hali mbaya ya kiuchumi ya timu hiyo, wameshindwa kupata mechi za kirafiki mpaka kufikia jana, lakini hajakata tamaa katika maandalizi yake ya kuelekea mchezo huo dhidi ya DRC.

"Vijana wana ari kubwa, wanafanya vema katika mazoezi yao, mipango bado inaendelea ya kusaka mechi za kirafiki, lakini ikishindikana tutajipanga kulingana na mazingira tuliyokuwa nayo," alisem Shime.

Wakati huo huo, mshambuliaji, Asha Hamza, anayetoka Kigoma Sisterz huenda akaukosa mchezo huo dhidi ya DRC kutokana na kuumia mkono katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika juzi jioni.

Asha ameteguka mkono wa kushoto na tayari amewekewa plasta ngumu.

# Michezo

Ijumaa Machi 29, 2019

Nipashe

## Ndoto za Solskajer zatimia



HABARI UK. 30



Straika wa Brazil, Roberto Firmino ambaye anaichezea Liverpool akijiandaa kupiga shuti katika mechi ya kirafiki dhidi ya wenzao wa Jamhuri ya Czech iliyochezwa mapema wiki hii. Brazil ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# AJIBU KUIKOSA ALLIANCE KESHO

### Hata hivyo Kocha Zahera asema ushindi utapatikana bila wasiwasi...

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga kilitua salama jijini Mwanza lakini kikiwa bila ya mshambuliaji wao tegemeo, Ibrahim Ajib, imeelezwa.

Yanga inatarajia kuwakabili wenyeji Alliance FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kuanza safari ya kuelekea Mwanza, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema kuwa alifikia uamuzi wa kumwondoa Ajibu katika programu ya mechi ya kesho kutokana na mshambuliaji huyo kutokuwa "fiti".

Zahera alisema kuwa Ajibu anasumbuliwa na maumivu kwenye nyama za paja na kutokana na hali hiyo nyota huyo ameshindwa kufanya mazoezi ya kutosha ili kucheza mechi hiyo ambayo mshindi anasonga mbele katika michuano hiyo.

Kocha huyo alisema kuwa anafahamu mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu wachezaji wa timu hizo mbili wanafahamiana.

"Tumeamua kumwacha Ajibu kwa sababu hayuko fiti, anaumwa, hajafanya mazoezi ya kutosha kucheza kwa ushindani Jumamosi," alisema kocha huyo ambaye hakuwa na timu yake wakati inafungwa bao 1-0 na Lipuli FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa Machi 16 kwenye Uwanja wa CCM, Samora, Iringa.

Naye Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, aliiambia gazeti hili kuwa wachezaji Andrew Vicent "Dante" na Raphael Daudi ambao walikuwa majeruhi wamepona na walijumuishwa katika safari hiyo.

"Kila mechi kwetu ni fainali, tunakwenda Mwanza tukifahamu tunakwenda kushindana ili kusaka ushindi, tunawaheshimu Alliance kama tunavyoziheshimu timu nyingine," alisema kiongozi huyo.

Mshindi wa mechi hiyo atatinga moja kwa moja hatua ya nusu fainali na atakutana na Lipuli ambayo imesonga mbele baada ya kuwafunga Singida United mabao 2-0.

Timu nyingine ambayo imetinga hatua ya nusu fainali ni KMC FC ya jijini ambayo nayo iliwafunga African Lyon magoli 2-0, huku mchezo mwingine wa michuano hiyo hatua ya robo fainali unatarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba kati ya wenyeji Kagera Sugar dhidi ya Azam FC.

## Aussems aipigia hesabu Mbao FC

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa kikosi chake kinajiandaa kukutana na ushindani katika mchezo wake dhidi ya Mbao FC utakaochezwa keshokutwa kwa sababu timu zote wanazokutana nazo "zinatamani kuwaharibia".

Aussems alisema hali hiyo inamfanya awaandae wachezaji wake kupambana katika dakika zote na kutokata tamaa hata pale wanapozidiwa.

"Mechi itakuwa ngumu, tumekuwa na matokeo mazuri katika michezo yetu iliyopita, hii inatufanya tuendelee kujiimarisha ili kulinda hali hii, hakuna mechi rahisi," alisema Mbelgiji huyo.

Hata hivyo kocha huyo alisema kuwa bado ubovu wa Uwanja wa Jamhuri watakaoutumia katika mchezo huo umekuwa ni changamoto kwa wachezaji wake.

Baada ya mechi hiyo, Simba itaingia kambini kuanza maandalizi ya kuikaribisha TP Mazembe katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Aprili 6, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

## Serengeti Boys yaenda Rwanda

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys) wamekwenda Rwanda kwa ajili ya kushiriki mashindano maalumu yatakayoshirikisha nchi nne tofauti, imeelezwa.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana kuwa kikosi cha Serengeti Boys kimeondoka na wachezaji 23 pamoja na viongozi nane.

Ndimbo alisema mbali na Serengeti Boys ambayo itatumia mashindano hayo kama sehemu ya maandalizi ya Fainali za Afrika za Vijana (AFCON U-17), timu nyingine zitakazoshiriki mashindano hayo ni pamoja na wenyeji Serengeti Boys na Cameroon.

Wakati huo huo, kikosi cha Timu ya Vijana ya Taifa ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes) kimekwenda Eritrea kucheza mechi ya kirafiki na wenyeji wao itakayofanyika keshokutwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >